# Nipashe

Jumatatu Desemba 28, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580443

MWANGA WA...

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US




**Guardiola asifia kiwango Man City**

UKURASA 20

**Kanisa** lamwombea mama wa JPM

UKURASA 4



**Askofu** Banzi kuzikwa kesho

UKURASA 10

# Majaliwa ashtukia ufisadi bandarini

• **Amsimamisha** kazi Mkurugenzi wa Fedha, Meneja matumizi... *Endelea ukurasa 2*



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza katika kikao na Waziri na Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Wajumbe wa Bodi ya Mamlaka ya Bandari Tanzania na Menejimenti ya Mamlaka hiyo, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU ) na Mkurugenzi wa Mashtaka (DCI) kwenye ukumbi wa Mamlaka ya Bandari jijini Dar es Salaam. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

## YALIYOMO


UKURASA WA 4

**SAKATA LA KINA MDEE, CHADEMA KIZUNGUMKUTI**

WAKATI jana ikiwa ni siku ya mwisho kwa wabunge 19 wa viti maalum CHADEMA...

UKURASA WA 5

**MADEREVA KUPELEKWA MOCHWARI KUSHUHUDIA MIILI WALIOPATA AJALI**

JESHI la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, linaandaa utaratibu wa kuwapeleka madereva mochwari...


## IGP kupambana wanaotishia viongozi

UKURASA 5




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play · Download on the App Store




## Mama adaiwa kumuua mwanawe apate ajira

UKURASA 2

MICHEZO **SVEN NA HESABU KALI KWA PLATINUM** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA



Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Joachim Wangabo, akishiriki zoezi la ubebaji mawe pamoja na wananchi kwa ajili ya ujenzi wa msingi katika Shule ya Sekondari Matai wilayani Kalambo, wakati wa ziara yake wilayani humo juzi. Alikabidhi mifuko 30 ya saruji kwa Mkuu wa Wilaya ya Kalambo, Carolius Misungwi, ili kukabiliana na upungufu wa vyumba vya madarasa vitano katika Shule ya Sekondari Mambwe. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

# Majaliwa ashtukia ufisadi bandarini

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amemwagiza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), kufanya ukaguzi maalum katika Bandari za Dar es Salaam, Mwanza, Mtwara, Tanga na Kyela kutokana na kuwapo kwa matumizi mabaya ya fedha za umma.

Katika hatua pia, amewasimamisha kazi Mkurugenzi wa Fedha wa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Nuru Mhando, pamoja na Meneja wa Matumizi ya Fedha wa mamlaka hiyo, Witness Mahela, ili kupisha uchunguzi wa tuhuma za matumizi mabaya ya fedha zinazowakabili.

Waziri Mkuu alichukua hatua hiyo baada kupokea ripoti ya ukaguzi maalum uliofanywa na CAG katika hesabu ya Bandari ya Kigoma kwa mwaka 2017/2018 na 2018/2019. Lengo la ukaguzi huo lilikuwa kujiridhisha kuhusu matumizi mabaya ya fedha za umma.

Waziri Mkuu alitoa agizo hilo, jana, katika kikao chake na Waziri na Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Bodi ya TPA na menejimenti ya mamlaka hiyo, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), kilichofanyika katika ofisi za TPA jijini Dar es Salaam.

Akiwa katika kikao hicho, Majaliwa alisema taasisi hiyo imebeba taswira ya uchumi wa taifa, lazima kazi ifanyike vizuri.

Pamoja na mambo mengine, Majaliwa aliitaka Bodi ya TPA ihakikishe mamlaka hiyo inafanyakazi kwa weledi na isisite kuchukua hatua kwa mtumishi atakayebainika kutenda makosa na isimbebe kwa namna yoyote.

Alisema miongoni mwa mambo yasiyoridhisha yanayofanywa na mamlaka hiyo ambayo yanaikosesha serikali mapato ni pamoja na msamaha wa kodi ya zaidi ya Shilingi bilioni mbili ilioutoa kwa kiwanda cha saruji cha Mbeya, licha ya kukataliwa na kamati ya misamaha.

Alisema licha ya kuongezeka kwa makusanyo, lakini kati ya fedha inayokusanywa ni asilimia 70 pekee inayoingia serikalini na kiasi kilichobaki kinaishia mifukoni.

Waziri Mkuu alisema: "Ripoti ya CAG ya Bandari ya Kigoma haijatufurahisha imeonyesha mambo mengi mabovu."

Alisema katika hali isiyokuwa ya kawaida TPA iliidhinisha malipo ya Sh. bilioni 8.2 kwenda Bandari ya Kigoma kwa ajili ya kwenda kufanya malipo mbalimbali, huku ukomo wa bandari hiyo ni Sh. bilioni 7.4.

Alisema fedha hizo zilitumika kufanya malipo yasiyostahili kwa watu mbalimbali akiwamo mfanyabiashara wa duka la ujenzi mjini Kigoma, Eliya Mtinyako, aliyelipwa zaidi ya Sh. milioni 900.

"Malipo haya yamefanyika huku kukiwa hakuna nyaraka zinazoonyesha kama alilipwa kwa sababu zipi kwani mfanyabiashara huyo aliyelipwa hakuwahi kutoa huduma yoyote kwa mamlaka hiyo na wala siyo mzabuni. Pia amelipwa bila ya kuwapo kwa nyaraka za madai," alisema Majaliwa.

Alisema licha ya upotevu huo wa fedha katika bandari hiyo ya Kigoma, pia Mhasibu wa Bandari hiyo, Madaraka Madaraka, alifuta madeni ya zaidi ya shilingi bilioni moja waliyokuwa wakidaiwa wateja bila ya kufuata taratibu na kuisababishia serikali hasara.

Kadhalika, Majaliwa alisema ripoti hiyo ya CAG imebainisha uwapo wa malipo hewa ya zaidi ya shilingi bilioni mbili ambazo zimelipwa bila ya kufuata taratibu za malipo na wahasibu walipoulizwa walidai ni maelekezo kutoka makao makuu ya TPA.

Alisema walipofanya ukaguzi walibaini uwapo wa hundi 150 ambazo tayari zimesainiwa na wahusika wote na zimebaki wazi na mtu yeyote anaweza kujaza jambo ambalo ni kinyume na taratibu za serikali kwa kuwa hazitakiwi kuwa hivyo.

"Huu ni mpango wa wizi, mamlaka kubwa kama hii hatuwezi kuacha hivi, hii fedha iliyopotea tungeweza kujenga zahanati, tungewapa TARURA wangejenga barabara nyingi tu. Mheshimiwa anapoelekeza fedha zipelekwe bandari ni kwa ajili ya kuboresha bandari yetu na lazima zitumike vizuri," alisema Majaliwa.

Kufuatia hatua hiyo, Waziri Mkuu amemwagiza DCI, Robert Boaz ahakikishe Mtinyako na Madaraka, wanatafutwa popote walipo na kukamatwa. Pia aliagiza watumishi wote waliosimamishwa kazi wachunguzwe haraka na ikibainika kwamba hawana hatia warejeshwe kazini na wakikutwa na hatia hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao.

Pia Waziri Mkuu alimwagiza Mkurugenzi wa TAKUKURU afanye uchunguzi kuhusu Kalibilo ambaye aliingiziwa kiasi kingi cha fedha bila ya kuwapo nyaraka zinazoonyesha sababu za mtumishi huyo kulipwa fedha hizo.

"Agosti anaonekana alilipwa shilingi milioni 55, Septemba shilingi milioni 53, Oktoba shilingi milioni 37 na Novemba shilingi milioni 19, lazima atafutwe popote alipo ijulikane fedha hizo alilipwa kwa ajili gani."

# Mama adaiwa kumuua mwanawe apate ajira

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

MKAZI wa Kijiji cha Mwenge, Kata ya Mtina wilayani Tunduru, mkoani Ruvuma, Neema Athumani (24), anashikiliwa na polisi kwa tuhuma za mauaji ya mtoto wake kwa kumwekea sumu ya panya kwenye soda.

Taarifa za tukio hilo zinadai kuwa mwanamke huyo alitekeleza mauaji hayo Desemba 24, mwaka huu, baada ya kuweka sumu ya panya kwenye soda na kumnywesha mtoto wake Rashfod Tariq, mwenye umri wa miaka minne.

Mashuhuda wa tukio hilo walisema kuwa baada ya mtuhumiwa huyo kutekeleza unyama huo, alichimba shimo na kwenda kumzika na baadaye kutoroka kijijini hapo.

Kwa mujibu wa taarifa hizo mtuhumiwa alikamatwa akiwa safarini kuelekea mkoani Arusha alikodai kuwa alikuwa anaenda kwa ajili ya kufanyakazi za ndani kutokana na ugumu wa maisha, baada ya mzazi mwenzake kumtelekeza na kukataa kumhudumia mtoto.

Akiongea na gazeti hili akiwa chini ya ulinzi wa polisi, mtuhumiwa huyo alikiri kufanya tukio hilo baada ya kupewa masharti na mwajiri wake wa mkoani Arusha kuwa kama anahitaji kazi aende bila mtoto.

"Nilimwekea sumu ya panya kwenye soda ili afe na mimi nipate nafasi ya kwenda kutafuta maisha mkoani Arusha baada ya mzazi mwenzangu kunitelekeza na mtoto tangu akiwa mdogo na kila ninapo mwambia aje amchukue mtoto wake amekuwa akikataa," alisisitiza Neema.

Kamanda wa polisi Mkoa wa Ruvuma, Simon Maigwa, alithibitisha kuwapo kwa tukio hilo na polisi bado inaendelea na uchunguzi wa chanzo cha tukio hilo.

Kamanda Mnaigwa alisema kuwa mtuhumiwa huyo anatarajiwa kufikishwa mahakamani baada ya kukamilika kwa taratibu za mahojiano ya awali.

TANGAZO

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

LATRA

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini

# TAARIFA KWA UMMA YA KUKANUSHA HABARI ZA KUPOTOSHA ZILIZOSAMBAA KUHUSU MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI (LATRA)

| NA | KUHUSU | HABARI YA KUPOTOSHA | UKWELI |
|---|---|---|---|
| 1 | Ukaguzi wa leseni za usafirishaji. | Maofisa wa LATRA wanakamata magari ya watu yasiyofanya biashara sehemu mbalimbali nchini. | LATRA hutoa leseni kwa magari ya biashara. Hii ni kwa mujibu wa Kifungu cha 5 (1)(b) cha Sheria Na. 3 ya mwaka 2019. Hivyo, ukaguzi hufanywa kwa magari ya biashara kuhakikisha watoa huduma wanazingatia takwa hili la kisheria. Wafanyakazi wa LATRA wanazingatia sheria hiyo. |
| 2 | Huduma kwa Wateja | Tukio la Afisa wa LATRA mkoa wa Lindi kugombana na dereva wa lori linaashiria kuwa hawana huduma nzuri kwa wateja. | Tukio hili haliwakilishi utendaji wa wafanyakazi wa LATRA. Wafanyakazi wa LATRA hufanya kazi kwa weledi na wamepata mafunzo ya Huduma kwa Wateja. Vilevile, kila mwaka, hupewa mafunzo ya Sheria, Kanuni na Miongozo ya utendaji kazi.<br><br>Kwa kuonyesha kuwa kitendo hicho hakikubaliki, LATRA ilimsimamisha kazi mfanyakazi huyo ndani ya saa 24. |
| 3 | Lengo kuu la Mamlaka | Lengo kubwa la LATRA si kuwalinda wasafirishaji, bali kuwakandamiza kutokana na kanuni zao ngumu. | Kwa mujibu Kifungu cha 6 cha Sheria ya LATRA Na. 3 ya mwaka 2019 jukumu kuu la LATRA ni kuboresha maisha ya Watanzania kupitia sekta ya usafiri ardhini kwa;<br>· kuimarisha ushindani na usalama,<br>· kulinda maslahi ya mtumiaji wa huduma na watoa huduma wenye ufanisi.<br>· Vilevile, kuhakikisha uwepo wa huduma za usafiri zenye uhakika na<br>· kutoa elimu kwa umma.<br><br>Changamoto iliyopo ni kuwepo kwa wasafirishaji wachache wasiotaka kutii sheria. |
| 4 | Ushirikishwaji katika Kutunga Kanuni za LATRA | Wakati wa utungwaji wa Kanuni mpya za LATRA za mwaka 2020 wasafirishaji hawakushirikishwa. | Wizara yenye dhamana na Uchukuzi, ikishirikiana na LATRA ilifanya mikutano kupata maoni ya Wadau mwezi Agosti, 2019. Mikutano hiyo ilifanyika kikanda katika mikoa ya Dar es Salaam (2), Arusha, Mwanza, Mbeya, na Dodoma.<br><br>Wasafirishaji walishiriki na maoni yao yalizingatiwa. |
| 5 | Zabuni za vifaa vya kufuatilia mwenendo wa mabasi (VTS) | Mchakato wa kupata Kampuni moja iliyopewa zabuni ya kuuza vifaa vya ufuatiliaji magari (Vehicle Tracking System) haukuwa sahihi. | Kampuni zinazofunga vifaa vya ufuatiliaji wa mwenendo kwenye mabasi ni nne (4). Ambazo ni<br>· Tera Technologies and Engineering Ltd,<br>· Easy Track,<br>· ICTpak na<br>· U-Track.<br><br>Kampuni hizi zilipatikana kwa njia ya ushindani kwa kuzingatia Sheria ya Ununuzi ya Umma kupitia mfumo wa TaNEPS.<br><br>Sababu ya kuwa na kampuni zaidi ya moja ni kuweka ushindani na kuwapa wasafirishaji wigo wa kuchagua kampuni wanayoiona inafaa zaidi. |
| | | VTS inatumika na LATRA kama kitega uchumi. | Mamlaka haipati fedha yoyote kutokana na VTS. Gharama hulipwa kwa kampuni za kufunga vifaa kwa ajili ya kununua kifaa na kulipia gharama za usimamizi za kila mwezi pamoja na mawasiliano (data). |
| 6 | Udhibiti wa mwendokasi hatarishi wa mabasi. | Basi lenye VTS linapozidisha mwendokasi uliopangwa wa kilomita 80 kwa saa, huachwa liendelee. Mwisho wa mwezi mmiliki anatozwa faini kulingana na mara ngapi dereva alizidisha mwendo. | Basi likizidisha mwendokasi kingo'ra ndani ya basi hulia kumtahadharisha dereva kupunguza mwendo. Aidha, kila basi lina speedomita inayomwezesha dereva kuona spidi ya gari. Vilevile, wamiliki wamepatiwa akaunti zinazowawezesha kuyaona mabasi yao kupitia simu zao za mkononi na kompyuta. Pale dereva na mwenye basi wanaposhindwa kuwajibika ndipo Mamlaka uingilia kati na kuchukua hatua ya kumtaarifu mmiliki na kuchukua hatua dhidi ya dereva na si mmiliki.<br><br>Na kwa zaidi ya mwaka mmoja sasa LATRA haiwachukulii hatua madereva kutokana na amri ya Mahakama Kuu. |
| 7 | Kanuni za LATRA | Kanuni za LATRA zina nguvu kubwa na zinaingiliana na majukumu ya Sheria ya Usalama Barabarani na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) | Kifungu cha 5 (1)(f) cha Sheria Na. 3 ya mwaka 2019 kinaipa LATRA jukumu la kudhibiti ubora wa vyombo vya usafirishaji ardhini. Jukumu hili ni tofauti na jukumu la Sheria ya Usalama Barabarani Sura 168.<br><br>Aidha, LATRA hakusanya levi kwa mujibu ya Kifungu Na. 35 (2) cha Sheria Na. 3 ya mwaka 2019. Hivyo, kutoingiliana kimajukumu na TRA. |
| 8 | Tozo ya Levi kwa waendesha Bodaboda | LATRA wanataka kuwasajili bodaboda waanze kuwatoza asilimia moja (1%) ya mapato ghafi. | LATRA inatoa leseni za bodaboda toka mwaka 2010 na haijawahi kuwataka bodaboda kulipa levi ya asilimia moja (1%).<br><br>LATRA ilipewa jukumu hili kupitia marekebisho ya Sheria ya Leseni za Usafirishaji ya mwaka 2009 yaliyofanywa kwa lengo la kurasimisha usafiri wa pikipiki kibiashara. |
| 9 | Maagizo ya Mh. Waziri Mkuu | Juni 30, 2019, Waziri Mkuu alielekeza kusitisha malipo ya vifaa vya ufuatiliaji magari (VTS). | Mh. Waziri Mkuu alisitisha malipo na kuitaka LATRA isimamie majadiliano kati ya wasafirishaji na watoa huduma kuangalia uwezekano wa kupunguza viwango vya ada za kila mwezi. Agizo hili lilitekelezwa na LATRA kwa kuwakutanisha wazabuni na wasafirishaji ambapo walifikia muafaka wa viwango vya kulipana kwa kila mwezi. |
| 10 | Ada ya Leseni za Malori | LATRA imepandisha ada ya stika kutoka Tshs 7,000 mpaka Tshs 185,000 kwa lori na Tshs 185,000 kwa trailer. Faini ni Tshs 500,000 kwa kila kosa. | Ada ya juu kabisa kwa leseni za malori ni Sh. 120,000.<br>Aidha, kuendesha gari la biashara bila ya leseni ni kosa kwa mujibu wa Kanuni ya 23 ya Kanuni za leseni za Usafirishaji (Magari ya Mizigo), za mwaka 2020 (Kiambatishi VI). Mtu atakaye dhibitika kufanya kosa atatozwa faini ya kati ya shilingi laki 2 na isiyozidi laki 5, au kifungo cha kuanzia miezi mitano na isizidi mwaka mmoja au vyote kwa pamoja. Na endapo mmiliki atakiri kosa na kukubali kulipa faini papo kwa hapo, hulipa nusu ya faini hiyo ambayo ni Sh. 250,000.<br><br>Hata hivyo, kanuni zinampa nafasi mwenye gari kukata leseni mwezi mmoja kabla ya leseni kuisha ili kuepuka usumbufu na leseni hiyo inaweza kukatiwa mahali popote nchini. |
| 11 | Kauli ya Mkurugenzi Mkuu wa LATRA kuhusu Tiketi Mtandao (e-Ticketing) | Mkurugenzi Mkuu wa LATRA kutoa kauli ya kusitisha matumizi ya mfumo wa Tiketi Mtandao wa National Internet Data Centre (NIDC). | Maneno hayo hayakutolewa na Mkurugenzi Mkuu wa LATRA. Aidha, LATRA haina uwezo wa kusimamisha matumizi ya mfumo wa Tiketi Mtandao kwani Mfumo huo umeanzishwa na Serikali kwa malengo mapana. |
| 12 | Madaraja ya leseni za udereva na vyeti vya uwezo | Majukumu ya Kifungu cha 19, 20, 23, 24 na 25 vya Sheria ya Usalama Barabarani kuhusu leseni ya udereva yanaingiliana na jukumu la LATRA kupitia kifungu cha 5(1) cha Sheria ya LATRA Na. 3 ya mwaka 2019. | Sheria ya LATRA Na. 3 ya mwaka 2019 inaipa Mamlaka uwezo wa kuthibitisha madereva wa kuendesha magari ya biashara ambayo yanadhibitiwa na Mamlaka. Utaratibu huo sio mgeni na una lengo la kuongeza usalama wa vyombo hivyo na ubora wa huduma zinazotolewa. |

HABARI KITAIFA

# Sakata la kina Mdee, CHADEMA viti maalumu bado kizungumkuti

**Na Elizabeth Zaya**

WAKATI jana ikiwa ni siku ya mwisho kwa wabunge 19 wa viti maalum CHADEMA kukata rufani ya kupinga kuvuliwa uanachama, pande zote mbili zimekaa kimya kuzungumzia kinachoendelea.

Desemba mosi, mwaka huu, wakizungumza na vyombo vya habari jijini Dar es Salaam, wabunge hao wakiongozwa na aliyekuwa Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake wa chama hicho (BAWACHA), Halima Mdee (pichani), walidai kwamba wangekata rufani kuvuliwa uanachama kwa Baraza Kuu la chama baada ya kushauriana na wanasheria wao.

Mdee alisema ndani ya siku 30, baada ya kutafakari na kushauriana na wanasheria wao watakuwa wamekata rufani hiyo, katika Baraza Kuu la chama hicho, huku akidai kwamba kwa kipindi chote abacho watakuwa wakisubiri uamuzi wa rufani wataendelea kuwa wanachama wa hiari na ving`ang`anizi kutokana na mapenzi waliyonayo kwa chama chao.

Hadi jana jioni ambayo ndiyo siku ya mwisho, siyo uongozi wa CHADEMA wala upande wa wabunge hao 19 waliokubali kuzungumza kuhusiana na sakata hilo, baada ya Nipashe kuwatafuta kwa njia ya simu.

Miongoni mwa viongozi wa CHADEMA waliotafutwa ni Katibu Mkuu, John Mnyika, hata hivyo, simu iliita bila kupokelewa.

Mkuu wa Kitengo cha Habari na Mawasiliano wa chama hicho, Tumaini Makene, alipoulizwa juu ya suala hilo la hatima ya rufani ya wabunge hao 19, alisema: "Kiongozi gani aliyekuambia mwisho wa rufani ni leo (jana), mtafute huyo huyo ndiye atakueleza."

Nipashe lilimtafuta aliyekuwa Makamu Mwenyekiti wa BAWACHA, Hawa Mwaifunga, kutaka kufahamu kama wamekata rufani hiyo, na kujibu: "Niko safari siwezi kufahamu ambacho kinaendelea, naomba umtafute Salome Makamba kwa sababu nafahamu Halima Mdee alifiwa, na Grace Tendega (aliyekuwa Katibu Mkuu wa Baraza hilo) yuko nje ya nchi," alisema Mwaifunga.

Hata hivyo, Salome naye alipotafutwa katika simu yake ya mkononi, hakupokea.

Desemba 20, mwaka huu, alipotafutwa na gazeti hili kufahamu kama




wamepokea rufani hiyo, Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa Chama hicho, John Mrema, alisema wanasubiri mpaka Desemba 27 (jana), wafunge milango ya rufani hiyo.

Kwa mujibu wa CHADEMA, kina Mdee wanatakiwa kukata rufani hiyo ndani ya siku 30 kuanzia siku ya kuvuliwa uanachama endapo watakuwa na nia ya kufanya hivyo.

## Kanisa lamwombea uponyaji mama wa Rais Magufuli

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

KANISA la International Assemblies of God (IEAGT) la mjini Shinyanga, limefanya ibada ya maombi maalumu ya kumwombea uponyaji mama mzazi wa Rais John Magufuli.

Askofu wa kanisa hilo, David Mabushi, alisema jana kuwa Rais John Magufuli, amekuwa akimuuguza mama yake kwa muda mrefu, hivyo ni wakati wa madhehebu mbalimbali kufanya maombi maalum ya kumwomba Mungu amponye.

Alieleza kuwa kanisa hilo limeamua kufanya maombi hayo maalumu ya kumwombea mama wa Rais Magufuli apone haraka, ili kumpatia nafasi kiongozi huyo kuendelea kuwatumikia Watanzania akiwa na furaha na mama yake kuwa mzima.

"Rais wetu amekuwa akimuuguza mama yake kwa muda mrefu sana na Watanzania wengi tumekuwa tukimsifu kwa kazi nzuri ambayo anaifanya, lakini tunasahau kumwombea na mama yake, ili apone haraka. Ni wakati wa kufanya maombi maalum kwa ajili yake," alisema Mabushi.

Katika hatua nyingine alimpongeza Rais Magufuli kwa kumtanguliza Mwenyezi Mungu katika mapambano ya maambukizi ya corona hadi taifa kupata uponyaji na sasa liko salama.

Nao baadhi ya waumini wa kanisa hilo, Haruna Mghuna na Veronica Mwita, walisema jambo la kumwombea mama yake Rais Magufuli ni la kheri ambalo litampatia furaha kiongozi huyo kuendelea kuwatumikia Watanzania akiwa na furaha.

NHC
SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA
TUNAJENGA TAIFA LETU

**TAARIFA KWA WAPANGAJI WA NYUMBA ZA NHC WANAODAIWA KODI NA MALIMBIKIZO**

1. Shirika la Nyumba la Taifa linawashukuru wapangaji wake walioweza kulipa kodi na malimbikizo yao baada ya kupewa notisi ya siku kumi na nne (14) ya kulipa kodi na malimbikizo wanayodaiwa. Aidha, wapo wapangaji wachache ambao bado wanadaiwa kodi na malimbikizo hadi sasa.
2. Kwa mara nyingine, Shirika linatoa siku thelathini(30) kwa wapangaji wanaodaiwa kodi na malimbikizo kufika katika ofisi za Shirika zilizo karibu nao ili kulipa kodi na malimbikizo wanayodaiwa.
3. Shirika linawashauri wapangaji wote kutumia fursa hii kulipa madeni yao na baada ya muda huu uliowekwa kukamilika, Shirika litatumia taratibu za kisheria kukusanya kodi na malimbikizo yanayodaiwa wapangaji ikiwemo kukamata na kupiga mnada mali za wapangaji ili kufidia kodi na malimbikizo yanayodaiwa. Aidha, baada ya muda huu kupita, Shirika halitasita kutangaza kwenye vyombo vya habari majina ya wadaiwa wote sugu ili umma ufahamu watu wanaokwamisha maendeleo ya Shirika na Taifa kwa kutokulipa kodi.
4. Tunashukuru wapangaji wote wanaotimiza wajibu wao wa kulipa kodi kwa wakati na kuliwezesha Shirika na Taifa kuwaletea maendeleo watanzania kwenye sekta ya nyumba.

**IMETOLEWA NA: OFISI YA MAWASILIANO NA HUDUMA KWA JAMII**
**NHC-MAKAO MAKUU**

**SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA**
**MAKAO MAKUU S.L.P 2977 | DAR ES SALAAM TANZANIA | SIMU: +255 22 2105001-5 | NUKUSHI: +255 22 2105000**
**BARUA PEPE: dg@nhctz.com | TOVUTI: www.nhctz.com**

## HABARI KITAIFA

# Madereva kupelekwa mochwari kushuhudia miili waliopata ajali

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

JESHI la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani wilayani Tunduru, mkoani Ruvuma, linaandaa utaratibu wa kuwapeleka madereva na wananchi mochwari kuangalia miili ya watu waliopoteza maisha, majeruhi wa ajali ili kushuhudia walivyoumia.

Jeshi hilo limesema linaamini kuwa utaratibu huo utawafanya madereva na wananchi hao kujifunza kuwa makini wanapokuwa kwenye vyombo vya moto barabarani.

Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani wilayani Tunduru, Mkaguzi Msaidizi wa Jeshi la Polisi, Anosisye Mwaipopo, alisema hayo wakati akiwaeleza wajumbe wa kamati ya usalama barabarani.

Akifafanua kuhusu taarifa hiyo, Mwaipopo alisema hali za majeruhi wengi ambao hukimbizwa kwa ajili ya matibabu hospitalini kwa asilimia kubwa hutazamwa na polisi na maofisa tabibu, baadaye ndugu zao huja kuwaona wakiwa wamekwisha rudishiwa baadhi ya viungo vilivyovunjika.

"Wapo madereva wengi ambao pasipo kuwa watii wa sheria wamepata ajali na kupoteza maisha, huku kukiwa na kundi kubwa la wananchi wenzetu ambao walikuwa wanatumia vyombo vilivyopata ajali, kama abiria waliopata vilema vya maisha na kubakia kuwa wategemezi wa familia zao," alisisitiza Mwaipopo.

Alisema kuna wakati polisi wanaposimamisha gari na kuingia ndani kwa ajili ya ukaguzi, hutokea baadhi ya abiria kuwalaumu askari kuwa wanawachelewesha na wakiondoka wapo ambao huwahamasisha madereva wakimbie ili wawahi kufika.

Akizungumzia wanavyopambana kuokoa maisha ya majeruhi na kuiandaa miili ya watu waliopoza maisha kutokana na ajali, Mganga Mkuu wa Wilaya, Dk. Wendi Robert, alisema bila maofisa tabibu kuwa na mioyo migumu, uwezekano wa familia zinazokumbwa na kadhia hizo zisingeweza kuwatazama wapendwa wao.

"Majeruhi wengi na watu waliopoteza maisha kwenye ajali nyingi mbalimbali barabarani hufikishwa kwenye vituo vya afya, zahanati na hospitalini wakiwa wamevunjika vibaya viungo vyao kiasi cha kutotazamika," alisema Dk. Robert.

# IGP kuwashughulikia wanaotishia viongozi

**Na Thobias Mwanakatwe**

JESHI la Polisi limeahidi kuchunguza na kuchukua hatua dhidi ya 'wasiojulikana' wanaodaiwa kuwatishia kuwaua viongozi wa CCM mkoani Iringa, akiwamo mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC), Salim Abri Asas.

Mkuu wa Jeshi la Polisi, IGP Simon Sirro, alisema hayo jana wakati akielezea kero iliyowasilishwa na mwananchi mmoja wa Iringa kufuatia kuendelea kwa vitisho kwa baadhi ya viongozi wa CCM wa mkoa huo. Mwananchi huyo akielezea kero hiyo kwenye kipindi cha Papo kwa Papo kinachoendeshwa na Katibu wa Itikadi na Uenezi Taifa wa chama hicho, Humphrey Polepole, alisema baada ya kumalizika kwa uchaguzi mkuu, viongozi wa chama wameendelea kutishiwa kuuawa na baadhi ya watu wasiojulikana.

Kufuatia kero hiyo, Polepole alimpigia simu IGP Sirro kusikia kauli ya Jeshi la Polisi ambaye alisema uchunguzi utafanyika haraka kuhusiana na jambo hilo na hatua zitachukuliwa kwa wahusika wote.

IGP Sirro aliwataka viongozi na wananchi ambao wanatishiwa, kuripoti kwenye vituo vya polisi ili ufuatiliaji uanze haraka.

Polepole alisema suala la vitisho kwa viongozi wa CCM Mkoa wa Iringa siyo la kupuuza hasa ikizingatia kuwa wakati wa uchaguzi, aliyekuwa Mwenyekiti wa wanafunzi wa vyuo na vyuo vikuu UVCCM Mkoa wa Iringa, Emmanuel Mlelwa, aliuawa mkoani Njombe.

Alisema, kwa kuwa jambo hilo limeshavifikia vyombo vya ulinzi na usalama ni matumaini ya CCM kwamba uchunguzi wa haraka utafanyika na wahusika kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

Polepole alisema ni jambo la kushangaza vitisho kuendelea, wakati uchaguzi umekwisha na wananchi wamekiamini Chama Cha Mapinduzi na kukichagua na kilichobaki ni kuwaletea maendeleo.

Alisema chama kwa upande wake kitaendelea kufuatilia kwa karibu jambo hilo ili viongozi wa CCM waendelee kubaki salama.


## NAFASI ZA SHULE

**Keland Nursery and Primary School iliyopo Salasala Rtd inatangaza Nafasi Za Awali Na Msingi. Mawasiliano : 0713327613.**


## KUPOTEA KWA VYETI



**HASSAN A. HASSAN** anatangaza kupotelewa kwa vyeti vifuatavyo,cha kidato cha nne chenye index namba **S1045-0233** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **DAR ES SALAAM** mwaka **2011** na cheti cha chuo **INSTITUTE OF TECHNOLOGY na TRANSCRIPT** chenye index namba **120121438617** kilichotolewa mwaka **2015**,yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**Polisi taarifa CD IR/RB/6887/2018**


The Guardian www.ippmedia.com

Nipashe MWANGA WA JAMII




For our Advertisement Customers

| Just pay for your Print advertisement | Get Free | | | |
|---|---|---|---|---|
| Size of Advertisement | Free E-Paper for One Month | | Free Social Media Post | |
| | The Guardian | Nipashe | Guardian or Nipashe | Guardian or Nipashe |
| Full Page | 10 E-Papers | 10 E- papers | 5 Posts | 5 Posts |
| 3/4 Page | 7 E- Papers | 7 E - Papers | 2 Posts | 2 Posts |
| 1/2 Page | 5 E- Papers | 5 E- papers | 2 Posts | 2 Posts |
| 3/8 Page | 3 E- Papers | 3 E- Papers | 1 Post | 1 Post |
| 1/4 Page | 2 E- Papers | 2 E- Papers | 1 Post | 1 Post |



For More Information Please Contact us:

0782 253 676 advertise@guardian.co.tz

1. This offer is Valid till 31st Dec 2020
2. Terms and conditions apply

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Namungo inawezekana zikijipanga dakika 90 za pili Caf

**WAWAKILISHI** wa Tanzania Bara katika michuano ya kimataifa, Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika, Simba na Namungo FC, bado wanakabiliwa na dakika 90 za mwisho kwenye raundi ya kwanza ya kinyang'anyiro hicho, ili kuweza kukata tiketi ya kusonga mbele.

Namungo ambayo inaiwakilisha nchi kwenye Kombe la Shirikisho Afrika, ikiwa nyumbani kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam, ilianza vizuri mechi yake ya kwanza kwa kupata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Al Hilal Obayed ya Sudan.

Hivyo, inachotakiwa kufanya katika mechi ya marudiano Januari 6, mwakani nchini Sudan, ni kuhakikisha inaulinda ushindi huo ama kwa kupata sare yoyote au kutokubali kupoteza kwa zaidi ya bao moja.

Ikumbukwe safari ya Namungo kutinga hatua ya makundi ya michuano hiyo bado ni ndefu, kwani hata kama itaitoa Al Hilal Obayed bado itakuwa ikikabiliwa na kucheza mechi ya mchujo dhidi ya timu itakayopangwa nayo kutoka zile zitakazotolewa kwenye hatua hii ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Lakini kwa upande wa Simba ambayo inapeperusha bendera ya Tanzania kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, ilianzia ugenini nchini Zimbabwe dhidi ya wenyeji wao, FC Platinum, na kukubali kipigo cha bao 1-0, hivyo inachokitaka ni ushindi tu wakati zitakaporudiana Januari 6, mwakani, katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Hata hivyo, kama Simba itafanikiwa kuitoa FC Platinum, itatinga moja kwa moja hatua ya makundi ya michuano hiyo, inayotarajiwa kuanza Februari mwakani, na kama itatolewa basi itaangukia kucheza mechi ya mchujo na timu kutoka Kombe la Shirikisho na endapo itapata matokeo ya jumla basi itatinga hatua ya makundi ya michuano hiyo ya pili kwa utajiri kwa ngazi ya klabu barani Afrika.

Kwa ujumla pamoja na Namungo kushinda mechi yake ya kwanza nyumbani, bado haiwezi kujihakikishia kuwa na nafasi ya kusonga mbele kabla ya kumaliza dakika 90 za pili kwenye mechi ya marudiano hapo Januari 6, mwakani.

Hivyo, kinachotakiwa kufanywa na wawakilishi wetu hao wawili, Simba na Namungo, ni kuzidi kuufanyia kazi upungufu uliojitokeza katika mechi zao zilizopita ili kujiimarisha zaidi kuelekea mechi za marudiano.

Tunatoa taadhari husuan kwa Simba, kuwa makini na mechi ya madrudiano kwani tayari ipo nyuma kwa bao moja, na endapo ikizembea na kuwaruhusu wapinzani wao kupata bao la ugenini, italazimika kushinda kuanzia mabao 3-1 ili kusonga mbele, hivyo huu ni mchezo mgumu sana kwao na si rahisi kama ambavyo wengi wanadhani.

Lakini wapinzani wao, tayari nao wameshafahamu udhaifu na uimara wa Simba, hivyo watacheza kwa tahadhari kubwa huku wakijilinda zaidi na kufanya mashambulizi ya kushtukiza ambayo mara nyingi huitia matatizoni safu ya ulinzi ya Simba.


Aidha, tunaikumbusha Simba kuwa makini zaidi ili kuepuka yaliyowakuta msimu uliopita baada ya kutoka suluhu ugenini dhidi ya UD Songo ya Msumbiji, lakini ikajikuta ikitolewa nyumbani baada ya wapinzani wao kufaidia na bao la ugenini kutokana na sare ya bao 1-1.

Nipashe tunaamini makocha wa timu zote mbili, kwa Simba, Sven Vandenbroeck na Namungo, Hemed Morocco, wameshabaini matatizo yalipo katika vikosi vyao na watayafanyia kazi kabla ya mechi za marudiano.

Zimebaki siku takriban tisa za kujipanga upya kabla ya timu hizo kushuka tena dimbani kwenye mechi za marudiano, hivyo tunataka kuona timu zote mbili zikisonga mbele na hilo litawezekana tu kama kutafanyika maandalizi ya kina, lakini mashabiki wakiungana na timu zao viwanjani kuzishangilia mwanzo mwisho.

Lengo letu ni kuona bendera ya nchi ikiendelea kupepea vema katika mashindano hayo na kuzidi kulitangaza soka la Tanzania, hivyo tunawatakia maandalizi mema wawakilishi wetu kimataifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Simba wakiamua Platinum itang'oka

**KWA** bahati nzuri Watanzania wengi walipata fursa ya kuiangalia mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika kati ya FC Platinum dhidi ya Simba kwenye runinga katika mchezo uliochezwa nchini Zimbabwe.

Hii ni tofauti na mechi iliyopita dhidi ya Plateau United ambapo wenyeji walikataa isionyeshwe, badala yake Wabongo walichoona ni mechi ya marudiano iliyochezwa hapa nchini.

Kwenye mechi iliyochezwa nchini Zimbabwe, Simba ilichapwa bao 1-0, hivyo ina deni la kushinda kuanzia mabao 2-0 na kuendelea ili kusonga mbele na kutinga hatua ya makundi kama ilivyowahi kufanya mwaka 2018, ilipoitoa Nkana FC kwa jumla ya mabao 3-2.

Simba ilichapwa mabao 2-1 nchini Zambia na kwenye mechi ya marudiano, Simba ilishinda mabao 3-1 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Kwenye mechi ya marudiano inayotarajiwa kuchezwa Januari 6, mwakani kama wachezaji wa Simba wataingia na morali na kujituma, basi hakuna kitakachoshindikana.

Ukiwaangalia FC Platinum si wazuri sana kama walivyokuwa Nkana FC wakati ule. Tatizo ni moja tu. Ni kwamba inavyoonekana wachezaji wa Simba kwa siku za karibuni wamekosa ari na kasi waliyokuwa nayo mwanzo.

Siku hizi wachezaji wa Simba hawakimbii, badala yake wanatembea uwanjani. Ikizidi sana ni kama wananyata hivi. Kwenye mechi iliyoonekana nchini Zimbabwe ni kwamba wachezaji wa Simba walionekana ni wazuri kwa mmoja mmoja kuzidi wapinzani wao, lakini wenzao walikuwa wanajituma, wanakimbia, wanafika maeneo husika kwa wakati sahihi, na wanatafuta nafasi.

Ni kama vile wachezaji wa Simba walikuwa wanajiona kama wanacheza na moja kati ya timu inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara na si timu ambayo imeshatinga hatua ya makundi mara tatu mfululizo.

Wakati wachezaji wa Platinum wakipanda mbele na kwa bahati mbaya wakinyang'anywa mpira, wachezaji wa Simba wanaanza kupasiana pasi fupi fupi zisizo za maana badala ya kupiga mpira mrefu sehemu ambazo kuna mapengo ya wachezaji waopanda mbele.

Hii ndiyo ilikuwa falsafa ya Simba ya mwaka 2018. Walikuwa wanacheza pasi fupi fupi pale wapinzani wanapokuwa nyuma ya lango, lakini wanapopanda na kunyang'anywa mpira, Simba wanafanya shambulizi la kushtukiza kwa pasi ndefu, wakikimbia kwa kasi na ndiyo iliwapa mabao mengi.

Tazama mechi za Nkana FC, JS Saoura, AS Vita, Al Ahly, utaona mabao mengi ya Simba ni ya mashambulizi ya kushtukiza.

Kwa sasa wachezaji wa Simba hawawezi kufanya mashambulizi ya kushtukiza kwa sababu hawakimbii. Sijajua sababu ni nini. Wanacheza kama wamelazimishwa. Wengi wanmlaumu Kocha Mkuu, Sven Vandenbroeck, kuwa na mifumo migumu na kusababisha wachezaji kushindwa kumudu.

Kwenye soka, inafika wakati mifumo ya kocha inafeli na sasa inatakiwa wachezaji ndani kutumia uwezo, jitihada na vipaji kuamua matokeo.

Ndiyo maana kwenye mechi iliyocheza Zimbabwe, baadhi ya mashabiki waliwakumbusha mno wachezaji kama Emmanuel Okwi, na wengine wakaenda mbali sana na kusema hata Benard Morrison mechi ile ilimfaa na angeweza kufanya kitu. Ilikosa mchezaji wa kuchukua mpira na kuamua kuanza kupasua na kwenda mbele kwa kasi akiingia ndani ya eneo la hatari ili kutengeneza mianya ya makosa kwa mabeki wa FC Platinum.

Nimeona viongozi wa Simba wakitoa kauli mbiu ya 'Vita ya Dar' kwenye mechi hiyo. Ni kweli, mashabiki wa Simba wanaweza kuwa chachu ya ushindi kwenye mechi hiyo, pamoja na mfumo wa kocha.

Lakini kama wachezaji wataendelea kucheza kwa kutembea na pasi fupi fupi zisizo na maana kama wako kwenye mazoezi itakuwa ni kazi bure na Simba haitoweza kufikia lengo.

Simba inaweza kutinga tu hatua ya makundi kama tangu mwanzo wa mchezaji, wachezaji wa Simba wataamua kulishambulia lango la FC Platinum kama nyuki, wakicheza mpira wa pasi ndefu zitakazopigwa kwenye mianya, ikichezesha wachezaji wenye kasi kama Luis Miquissone na Morrison, pia wachezaji wa Simba muda wote wawe wanakimbia.

Kingine ni kwamba wanajaribu kupiga mashuti makali wanapofika karibu na lango badala ya kutafuta mtu wa kumpasia wakati tayari mtu yupo langoni.

# Moto wateketeza maduka Sikukuu Krismasi

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

MOTO uliozuka usiku wa mkesha wa Sikukuu ya Krismasi umeteketeza maduka matano, saluni, mgahawa katika Kata ya Kayanga, wilayani Karagwe, mkoani Kagera.

Mkuu wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji mkoani Kagera, Hamisi Dawa, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo ambalo alisema lilitokea majira ya 5:49 usiku Desemba 26, mwaka huu.

"Tukio limetokea pale Kayanga mjini duka moja lilianza kushika moto na kusambaa kwa mengine, maaskari wetu walifika eneo la tukio na kupambana kuzuia moto usiendelee," alisema Dawa.

Alisema moto huo uliteketeza maduka matano, saluni moja na mgahawa, hata hivyo hasara iliyosababishwa na moto huo bado haijajulikana.

Aliongeza kuwa walipata taarifa za tukio hilo kupitia kwa Mkuu wa Wilaya ya Karagwe, Godfrey Mheluka na mwananchi wema.

Nipashe lilizungumza na baadhi ya mashuhuda wa tukio hilo akiwamo Mwajuma Aboubakary, ambaye alisema wakati maduka hayo yanateketea hapakuwapo na gari la zimamoto, huenda lingekuwapo wafanyabiashara wangeokoa mali zao.

Alisema askari wa zimamoto walifika eneo la tukio, lakini hawakuwa na vitendea kazi ikiwamo gari za kuzima moto.

Shuhuda mwingine ni Sajenti Suleiman, alisema tatizo la ubovu wa gari la zimamoto ni kubwa na kwamba mali za wananchi zinateketekea kwa kukosa vitendea kazi.

Akizungumzia tukio hilo, Mkuu wa Wilaya ya Karagwe, Godfrey Mheluka, alikiri kwamba gari la zimamoto lipo kwenye matengenezo na kwamba litatengemaa hivi karibuni.

Alisema gari hilo litakapotengenezwa litasaidia kupunguza majanga ya moto na kuahidi kwamba wiki mbili zilizopita alifanya mawasiliano kuhusu hilo gari na kuambiwa litakuwa tayari hivi karibuni.

## Wanafunzi wasitisha masomo kwa kukosa barabara

**Na Thobias Mwanakatwe**

WANAFUNZI wa Shule ya Sekondari ya Ivuma, wilayani Momba mkoani Songwe, wamelazimika kusitisha masomo kutokana na kukosekana kwa barabara.

Diwani wa Kata ya Mkomba, Moses Sinkamba, alimweleza jana Mbunge wa Jimbo la Momba, Condester Sichalwe, katika ziara yake ya kusikiliza kero za wananchi.

"Mheshimiwa mbunge, wananchi wako tupo kisiwani hatuelewi tufanye nini na hizi barabara kwani juzi, hapa tulimpoteza mama aliyekuwa anajifungua, tulikuwa tunamkimbiza hospitalini, lakini kutokana na ubovu wa miundombinu na kujaa kwa Mto Nyamba akafia njiani, kwa kweli naongea kwa uchungu mkubwa," alisema Sinkamba.\

Alisema ili kuwasadia wanafunzi kuendelea na masomo shule zitakapofunguliwa Januari mwakani na kunusuru vifo vya wajawazito, wangeomba serikali kuwajengea daraja la kiteputepu wakati inajipanga kujenga daraja la kudumu.

Akijibu malalamiko hayo, mbunge huyo alisema amepokea kero hiyo na zingine kuzishuhudia kwa macho na kwamba atahakikisha anapaza sauti kwa mamlaka zinazohusika ili kuzipatia ufumbuzi.

Sichalwe alisema ili kutatua haraka kero ya barabara katika jimbo lake, kunahaja kwa serikali kuangalia uwezekano wa kuzihamishia baadhi ya barabara zinazohudumiwa na Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini (TARURA), kwenda Wakala wa Barabara nchini (TANROAD).

Sichalwe alisema kuwa Jimbo la Momba lenye kata 42 na vijiji zaidi ya 100, TARURA wanahudumia barabara 57, huku TANROAD ikihudumia barabara mbili pekee.

## Wafugaji watakiwa kuchanja mifugo

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amewaagiza wafugaji nchini kuchanja mifugo yao ili kuepusha magonjwa ya milipuko.

Agizo hilo alilitoa baada ya kutembelea Taasisi ya Chanjo Tanzania (TVI), Kibaha mkoani Pwani.

Ndaki alisema Tanzania ina chanjo za mifugo za kutosha, hakuna haja ya kuzembea na kuacha mwanya wa magonjwa kushambulia wanyama.

Alisema kuzingatia suala hilo la chanjo kutasaidia kuwa na mazao bora yatokanayo na wanyama na Tanzania kuwa na mifugo bora inayokidhi soko la kimataifa.

"Tunataka nchi yetu iende kwenye ubora badala ya kuwa na mifugo mingi isiyo na bora, kwa sasa tunataka kubadilika ili tupate nyama na maziwa yenye viwango tuuze katika soko la kimataifa," alisema Ndaki.

Alisema ni muhimu kwa wafugaji kuhakikisha wanakuwa na mifugo iliyo bora ili wauze kwa bei yenye tija na wanufaike kiuchumi na taifa pia lipate mapato ya kutosha kupitia biashara ya mifugo.

Katika ziara hiyo, Ndaki alipongeza hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha chanjo wilayani Kibaha na kwamba kitakapoanza kufanya kazi kitaongeza wigo wa uwapo wa chanjo nyingi nchini.

Alisema uwapo wa viwanda vya kuchinja na kuchakata nyama nchini kutakuza biashara ya mifugo na kuongeza wigo wa soko la mazao hayo.



# Mradi wa zaidi ya bil. 10/- kunufaisha wakulima mboga

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

OFISA ufuatiliaji na tathmini wa mradi wa viungo Zanzibar wenye thamani ya Euro milioni tano (Sh. bilioni 14.3) unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya, Ali Abdalla Mbarouk, amesema, watahakikisha mradi huo unatatua tatizo linalowakabili wakulima wa mboga, matunda na viungo, ili kuzalisha bidhaa bora na zenye thamani.

Akizungumza katika mkutano wa kuutambulisha mradi huo kwa taasisi za serikali alisema, kupitia mradi huo watafanya jitihada kuweka sera zitakazomwezesha mkulima kufikia anayoyatarajia.

Alisema, kwenye kilimo kuna matatizo ya maradhi, vitendea kazi, wakulima kukosa mbinu za kuhifadhi, na kwamba watayatatua kwa kuhakikisha kunakuwa na ukuaji wa uchumi shirikishi ndani ya jamii.

"Kwa kweli huu mradi umekuja kuwakomboa wakulima wetu, tutaongeza thamani ya mazao na wingi wa bidhaa hizo kwa ajili ya masoko, hii itasaidia ukuaji wa uchumi kwenye jamii yetu," alisema.

Alisema, watatumia mabwana na mabibi shamba angalau 400, ili wawafundishe wakulima hao namna ya kulima, kuzalisha pamoja na kukabiliana na matatizo ambayo yanarudisha nyuma maendeleo ya kilimo. Alisema, watahakikisha wakulima hao wanazingatia mabadiliko ya tabianchi katika kuendeleza shughuli zao za kilimo, ili wasiathirike na hali hiyo itakapojitokeza.

"Tutatoa elimu kwa wakulima hao wajijenge wenyewe kwanza kwa kula chakula wanachozalisha kisha kinachozidi ndipo wakiingize katika biashara," alisema.

Alisema, watahakikisha hali ya chakula na lishe zinaboreshwa kwa mkulima, ili awe na afya bora itakayomwezesha kufanya kazi zake vizuri zaidi. "Tutatoa elimu kwa wakulima hao wajijenge wenyewe kwanza kwa kula chakula wanachozalisha kisha kinachozidi ndipo wakiingize katika biashara," alisema.

Mrajis wa asasi zisizo za kiserikali, Halima Kahamis Ali, alisema kuwa, mradi huo utakuwa na manufaa makubwa katika jamii, kwa kuwa kilimo ndicho kitakachowapatia ongezeko la chakula.

Naye Mtekelezaji wa Mradi kwa upande wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA), Arafa Abdallah Juma, alisema kuwa ipo haja kwa taasisi za serikali na binafsi kushirikiana pamoja katika kutekeleza mradi ipasavyo kuhakikisha wanafanikiwa lengo walilolikusudia.

Mratibu wa TAMWA kisiwani Pemba, Fat-hiya Mussa Said, alisema, mradi huo unaotekelezwa kwenye asasi za binafsi Unguja na Pemba ambao unasimamiwa na serikali ni wa miaka minne.

Kwa upande wa washiriki wa mkutano huo walishukuru ujio wa mradi huo na kusema kuwa utawasaidia wakulima wengi, jambo ambalo litawaongezea kipato.

Mradi huo unatekelezwa na TAMWA Zanzibar, Jumuiya ya Kuhifadhi Misitu asili Pemba (CFP) na Shirika la PDF la Dar es Salaam na unasimamiwa na serikali.


MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

**KUHUSU TARATIBU ZA UBORESHAJI WA MASHINE ZA RISITI ZA KIELEKTRONIKI**

Kwa kuzingatia TAARIFA KWA UMMA, iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania ("TRA" au "Mamlaka") ya mnamo tarehe **7 Disemba 2020,** ikiwaelekeza walipakodi kufanya maboresho ya Mashine za Risitiza Kielektroniki, yaani, Electronic Fiscal Device (EFD), zisizokuwa na uwezo wa kutoa risitizinazowezesha kufanya uhahiki kuendana na matakwa ya mfumo mpya wa kuwasilisha ritani za kodi. Mamlaka inapenda kuwashukuru wananchi wote walioitikia wito huu na tunatarajia kwamba maboresho haya yatamali zika ndani ya muda wa **siku thelathini (30)** zilizotolewa tangu tarehe **7 Desemba 2020**. Aidha, tunaendelea kuwahimiza wote ambao bado wajitokeze mapema iii kuepusha usumbufu unaoweza kujitokeza, ikiambatana na adhabu kwa mujibu wa Sheria, kwa kutobadilisha mashine za EFD mapema kama ilivyoelekezwa.

Kabla ya kuanza zoezi hili la mabadiliko Mamlaka ilizifanyia majaribio modeli zote za mashine zinazotumika iii kuainisha mashine zinazoweza kubadilishwa na zile ambazo hazina uwezo wa kubadilishwa. Ili kuepusha usumbufu unaoweza kujitokeza, tunawashauri wafanyabiashara ambao bado hawajafanikiwa kubadilisha mashine zao kuziwasilisha TRA kwa ajili ya kubadilishwa au kupatiwa taarifa sahihi ya nini cha kufanya kama mashine zao haziwezi kubadilishwa kwa sababu yoyote ile. Inafahamika kwamba Mamlaka inazo Ofisi na vituo nchi nzima ambazo zitakuwa tayari kuwasaidia walipakodi iii kufanikisha mabadiliko hayo kufanyika.

Tunaendelea kuwakumbusha kuwa fedha za kununua mashine mpya zitagharamiwa na Serikalikwa kuruhusiwa kudai kwenye ritani za Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ambazo huwasilishwa kila mwezi kwa mujibu wa **Jedwali la Saba (7) la Kanuni za Usimamizi wa Kodi za Mwaka 2016.** Kwa wale ambao hawajasajiliwa na VAT, gharama za kununua mashine zitagharamiwa kwa kupunguzwa chini ya **Kifungu cha 11 (2) cha Sheria ya Kodiya Mapato, SURA 332.**

Tunaendelea kuwahimiza walipakodi kutimiza agizo la uboreshaji wa mashine zao ndani ya muda husika iii kuepuka adhabu na usumbufu usi o wa lazima. Vile vile, tunawahimiza wafanyabishara kutekeleza wajibu wenuwa kutoa risiti sahihi za EFD,kwa upande mmoja, na kwa upande mwingine, wanunuzi wa bidhaa na huduma, kutakiwa kudai risitiza EFD kama ilivyo matakwa ya Sheria.

**"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"**

**Imetolewa na:**
**IDARA YA HUDUMA NA ELIMU KWA MLIPA KODI**


# Wachimba madini kudhibiti wizi wa dhahabu

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

SIKU chache baada ya Waziri wa Madini, Doto Biteko, kufanya ziara ya kushtukiza katika Soko la Madini ya Dhahabu Mwime, Kata ya Zongomela wilayani Kahama, mkoani Shinyanga na kubaini utoroshwaji mkubwa wa madini hayo, Chama cha Wachimbaji Wadogo wa Madini (SHIREMA), kimesema kimejipanga kudhibiti wimbi hilo.

Desemba 24, 2020, Waziri Biteko, alifanya ziara ya kushtukiza katika Soko la Mwime na kubaini utoroshwaji wa dhahabu unaofanywa na wafanyabiashara kutoka jijini Dar es Salaam wakishirikiana na soko hilo jambo ambalo lilimkera na kukamata watu 11 waliohusika ikiwamo kuwasimamisha kazi ofisa madini na mwenyekiti wa soko hilo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mwenyekiti wa SHIREMA, Joseph Nalimi, alisema ubadhirifu huo unatokana na watu wasiopenda maendeleo ya nchi.

Alisema hali aliyoikuta waziri katika soko la Mwime haitajitokeza tena na kwamba chama hicho kwa sasa kimejipanga kushirikiana na Tume ya Madini, kupambana na watoroshaji na kuwachukulia hatua wanaotaka kuharibu sifa ya soko hilo.

Aliwaambia waandishi wa habari kuwa kwa hali hiyo, watu watakaofanya biashara ya dhahabu nje ya soko, watachukua hatua kali kabla ya serikali kuwachukulia hatua na kuongeza kuwa kwa sasa atahakikisha anafanya ziara za mara kwa mara kwa wamiliki wa mialo, ili dhahabu wanazozalisha kabla hazijaingia sokoni ziwe zimesajiliwa kukomesha utoroshaji.

Aliwataka wachimbaji wadogo wawafichue watu wanaofanya ubadhirifu ili hatua kali zichukuliwe dhidi yao, ili kukomesha hali hiyo huku akimwahidi Waziri Biteko kuwa wakati mwingine akirudi Kahama hatakumbana na hali aliyoikuta.

# Kifafa mimba tatizo kwa wajawazito

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

KIFAFA cha mimba na kutokwa damu nyingi wakati wa kujifungua ni miongoni mwa sababu zinazochangia ongezeko la vifo vya wanawake katika Mkoa wa Mwanza. Hayo yalibainishwa hivi karibuni na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Dk. Thomas Rutachunzibwa, katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC).

Alisema wajawazito wengi wanapoteza maisha kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo kifafa cha mimba na kutokwa damu nyingi wakati wa kujifungua.

Aidha, alisema wanakabiliwa na tatizo la upungufu wa watumishi, fedha, vifaa na uwajibikaji mdogo katika ngazi zote.

# Chama chalaani utoroshaji madini njia za panya

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

CHAMA cha Wachimba Madini Wadogo mkoa wa kimadini wa Kahama (SHIREMA), kimeeleza kuchukizwa na baadhi ya wafanyabiashara wanaowarubuni wenzao kuwauzia dhahabu kwa njia za panya, badala ya kuifikisha kwenye masoko yanayosimamiwa na serikali.

Mwenyekiti wa chama hicho, Joseph Nalemi, alitoa angalizo hilo baada ya hivi karibuni kuibuka kikundi cha wafanyabiashara wa madini 11 kutoka Dar es Salaam, waliofika katika mgodi mdogo wa Kabera Gold Mine na kuwarubuni wachimbaji kuwauzia madini kwa bei wanazopanga wenyewe na kusababisha wachimbaji hao kutorosha madini kwa njia za panya.

Nalemi alibainisha hayo jana wakati akizungumza na vyombo vya habari katika soko la madini Mwime Ilindi, lililoko katika Halmashauri ya Mji wa Kahama, na kusema hawatakubali kuona baadhi ya wafanyabiashara wakiendelea kuwarubuni wachimbaji kutorosha madini na kusababisha serikali kukosa mapato.

Alisema kuwa, serikali imeweka mazingira mazuri kwa wachimbaji wadogo kwa kuondoa baadhi ya kodi zilizokuwa zikiwakwamisha ili kila mmoja anufaike, lakini kumeibuka kikundi cha wafanyabiashara wachache na kuwahadaa kwa bei wanazopanga kumesababisha kutorosha madini.

"Miaka ya nyuma kabla ya serikali kuweka mazingira wezeshi ukipata dhahabu unakaa nayo kama vile una bangi ndani muda wote umejaa wasiwasi nakwenda kuuza mahala ambapo hapaeleweki na kwa bei ya hasara," alikumbusha Nalemi.

Aliwataka wachimbaji kuhakikisha kila mmoja anajaza fomu ya kiwango cha dhahabu anachokipata wakati akiona mawe yenye dhahabu kabla ya kwenda kuchenjua na kuuza kwenye soko la madini ili kundoa usumbufu unaojitokeza wakati wa uuzaji.

James Chanya, mchimbaji kutoka Kabera Gold Mine alisema, ili kukomesha tabia hiyo iliyoibuka sasa, kila mchimbaji anatakiwa kuwa mlinzi na mwenzake na akibaini kuwapo kwa baadhi ya watu hao kutoa taarifa kwenye uongozi ili kudhibiti mapema.

Waziri wa Madini, Doto Biteko, alifanya ziara ya kushtukiza katika mgodi mdogo wa Kabera Gold Mine na kubaini utoroshaji wa dhahabu kwa njia za panya na kusababisha wafanyabiashara 11 kukamatwa kwa kuwarubuni wachimbaji na kufuta leseni mbili za ununuzi wa madini.

# Wawekezaji waiomba serikali kuangalia upya tozo za mifugo

**Na Mbaraka Kambona,** LONGIDO

MKURUGENZI wa kiwanda cha kuchakata mazao ya mifugo cha Eliya Food Overseas, Shabbir Virjee, ameiomba serikali kupitia upya na kupunguza kodi na tozo za mifugo ili waweze kushindana vyema katika soko la kimataifa na nchi jirani kama Ethiopia, Kenya, Somalia na Uganda ambazo kodi zao ni ndogo na zinawawezesha kununua na kuuza mifugo pamoja na mazao yake kwa bei nzuri.

Virjee alitoa ombi hilo kwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul, alipotembelea shughuli zinazofanywa katika kiwanda hicho cha kuchakata mazao ya mifugo kilichopo Kijiji cha Namanga Mpakani, wilayani Longido, mkoani Arusha, Desemba 24.

Kwa mujibu wa Virjee, kwa sasa wanalipa kodi zisizopungua tano kabla ya kusafirisha mazao ya mifugo nje ya nchi, jambo ambalo alisema linawafanya wasiweze kushindana vizuri katika soko kwa sababu ya bei yao kuwa juu kutokana na kodi wanazolipia hapa nchini.

"Changamoto inayotukabili sisi ni kodi, tunalipa kodi zisizopungua tano, tunalipa kodi kwa Wizara ya Kilimo Sh. 50 kwa kilo, Bodi ya Nyama tunalipa asilimia moja ya thamani, BAKWATA tunalipa kwa ajili ya kibali cha Halal, tunalipa kodi kwa vibali vingine, na tunalipa asilimia 0.1 ya kodi ya mionzi, kila hatua tunalipa kodi ambazo kusema ukweli zinatufanya tushindwe kushindana na nchi jirani ambazo kodi zao ni ndogo," alisema Virjee.

Alitaja tatizo lingine ni kutopatikana kwa wanyama kama malighafi katika kiwanda hicho, huku akiiomba serikali kuwasaidia ili waweze kupata wanyama wengi ili kiwanda kiwe na uhakika wa malighafi.

"Wafugaji wengi wanakwenda kuuza mifugo yao nchini Kenya kwa sababu ya bei nzuri huko, tunaomba tusaidiwe ili tuweze kupata malighafi ya uhakika, sisi hapa tunachinja kwa siku mbuzi 2,000 na ng'ombe 400, hivyo unaweza kuona kuwa tunauhitaji mkubwa wa kuwa na uhakika wa malighafi ya kutosha kila siku," aliongeza Virjee. Alisema kama hali itaendelea hivyo uendeshaji wa kiwanda hicho utakuwa mgumu kwa sababu watashindwa kushindana katika soko la ndani hata nje, huku akisema lengo la kiwanda hicho ni kutoa ajira kwa Watanzania wasiopungua 150.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul, kwa upande wake aliwapongeza wawekezaji hao kwa jitihada kubwa walizozifanya kuwekeza kiwanda hicho ambacho kinatekeleza azma ya Rais John Magufuli ya kuona Tanzania inakuwa nchi ya viwanda na aliwahakikishia changamoto zao amezichukua na zitafanyiwa kazi.

"Nakuagiza Katibu Mkuu, Prof. Gabriel uunde timu itakayokuja kufuatilia ili kubaini hizo changamoto zote ikiwamo kwa nini wafugaji wanapeleka mifugo yao kuuza nje ya nchi na taarifa hiyo itufikie haraka ili tuweze kuishauri serikali kutatua changamoto hizo mapema," alisema Gekul.

Pia Waziri Gekul alimwagiza Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Prof. Elisante Ole Gabriel, kuangalia kwa namna gani Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO), inavyoweza kusaidia kutatua changamoto ya upatikanaji wa malighafi katika kiwanda hicho.

"Hiki kiwanda ni lazima tukilinde, tufanye kila linalowezekana kukilinda, ikiwamo kutoa elimu kwa wafugaji kujua uwepo wa kiwanda hiki na faida zake, ili waweze kujua kumbe wanaweza kuuza ng'ombe wao hapa hapa nchini bila kukimbilia nchi nyingine," aliongeza Gekul.

Aidha, alisema wizara itaendelea kuwawezesha wafugaji kupitia vituo vya uhimilishaji hapa nchini kuwapatia mbegu bora zitakazowasaidia kupata ng'ombe wazuri watakaowawezesha kupata kipato kizuri kupitia viwanda vinavyochakata mazao ya mifugo nchini.



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul (katikati), akiwa na wafugaji baada ya mkutano wao na Naibu Waziri huyo, uliofanyika mnada wa mifugo Kijiji cha Orendeke, Namanga Mpakani, wilayani Longido, mkoani Arusha hivi karibuni. **PICHA: MBARAKA KAMBONA**

# Wahalifu watumiwa ujumbe wa hadhari

**Na Steven William,** MUHEZA

JESHI la Polisi mkoani Tanga limeahidi kuimarisha ulinzi wakati wa mkesha wa Sikukuu ya Mwaka Mpya na kuwaonya wavunjifu wa amani, kubadili mienendo yao.

Aidha, limewaonya wenye nia ya kuchoma moto matairi barabarani na kulipua baruti kuwa watashughulikiwa kikamilifu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Blasius Chatanda, alitoa hadhari hiyo, jana, wakati akizungumza na Nipashe kuhusu kuimarisha ulinzi katika kusherehekea Sikukuu ya Mwaka Mpya.

Alisema polisi imejipanga katika ulinzi mkesha wa sikukuu hiyo na kwamba wananchi katika mkoa huo watasherehekea kwa amani.

Chatanda alitoa onyo kwa wale watu wenye tabia ya kujifanya wababe kuleta fujo na hivyo kukera wengine, akiwataka wasifanye hivyo maana wataishia mikononi mwa polisi kisha kufikishwa mahakamani.

Alisema ulinzi utaimarishwa katika makanisa yote usiku na mchana ambako waumini watakuwa katika ibada ya sikukuu hiyo.

Chatanda alisema kutakuwa na doria ya polisi wa miguu, magari na pikipiki katika wilaya zote za mkoa huo kwa ajili ya kulinda amani, kuhakikisha wananchi wanasherehekea Mwaka Mpya kwa utulivu.

Amewaonya madereva wa vyombo vya moto ambao watabainika wamelewa na kusababisha ajali, watakamatwa na kuwekwa mahabusu na kupelekwa mahakamani na pia leseni zao kufungiwa.

Chatanda aliwataka wazazi wenye watoto wadogo wasiwaruhusu kwenda kutembea wenyewe siku ya mkesha wa mwaka mpya na badala yake watoke nao.

Pia, alipiga marufuku watoto kwenda peke yao katika fukwe za bahari kama vile Pangani, Tanga Mjini na maeneo mengine kwa kuwa ni hatari.




Mkuu wa Wilaya ya Mbulu, Dk. Chelestino Mofuga (kushoto), akiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, Hatson Kamoga pamoja na Mbunge wa Jimbo hilo, Flatei Massay, wakipokea msaada wa mashuka 25 na vitanda 8 na magodoro kutoka kwa Meneja wa NMB Tawi la Mbulu, Adamu Mwaisumo (kulia). Benki ya NMB ilikabidi vifaa hivyo, mwishoni mwa juma kwa ajili ya Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu vyenye thamani ya Sh. milioni tano. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Askofu Banzi kuzikwa kesho

**Na Steven William,** MUHEZA

WAUMINI wa Kanisa Katoliki Jimbo la Tanga na viongozi wao wanajiandaa kwa mazishi ya Askofu wa Jimbo la Tanga, Mhashamu Antony Banzi, yatakayofanyika kesho jijini Tanga.

Kwa mujibu wa taarifa zilizotolewa na Baraza la Maaskofu Tanzania (TEC), Askofu Banzi, atazikwa kesho jimboni kwake.

Mbunge mstaafu wa Jimbo la Muheza, Hebert Mntangi, ni miongoni mwa waumini hao, ambaye katika mazungumzo yake na Nipashe, alisema anasali eneo la Majengo Shimoni na kwamba alimfahamu vizuri Askofu Banzi na kutoa pole kwa Wakatoliki wote, mapadri, ndugu, familia, marafiki na watawa wa kanisa hilo.

Askofu Banzi alifariki dunia Desemba 20, wakati akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), jijini Dar es Salaam. Alifariki kutokana na maradhi ya koo.

Baadhi ya waumini wa kanisa hilo wilayani Muheza, Mage Samwel, alisema wengi wameshtushwa na kifo cha Askofu Banzi, ambaye walimhitaji aendelee kuliongoza kanisa.

Mage alisema alipata taarifa za kuumwa kwa Askofu Banzi na juhudi za baadhi ya makanisa mkoani hapo, kuchanga fedha za matibabu ili kumpeleka nje ya nchi kwa matibabu zaidi.

Alisema Askofu Banzi atakumbukwa kwa kufanya kazi kubwa ya kulitumikia kanisa hilo kwa miaka mingi hasa katika jimbo hilo.

Muumini mwingine wa kanisa hilo, Augustino Michael, alisema baada ya kupata taarifa ya kifo cha Askofu Banzi, wengi waliamini kuwa maisha ya binadamu yana mwisho lakini, atakumbukwa kwa kuunganisha kanisa na kuliwezesha kuwa na umoja na mshikamano.

# Jumuiya ya Wazazi yakumbushwa

**Na Yasmine Protace,** MKURANGA

WAJUMBE wa Jumuiya ya Wazazi CCM, Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, wametakiwa kufanya vikao vya kikatiba pamoja na ziara katika ofisi za serikali za vijiji, kata na shuleni, ili kuangalia matatizo yanayowakabili wanafunzi hasa wa kike.

Katibu wa Jumuiya hiyo, Emmanuel Mtatiro, alikumbusha hayo katika mkutano ulioandaliwa na Jumuiya ya Wazazi CCM.

"Wajumbe mnatakiwa mjiandae na mkutano mkuu wa uchaguzi mwakani na pia nawasisitiza kufanya vikao vya kikatiba na ziara katika ofisi za serikali za vijiji, kata ikiwamo pia kuzuru shule kwa kuangalia changamoto zinazowakabili wanafunzi wa kike," alisema.

Mwenyekiti wa jumuiya hiyo, Hami Mtutu, akizungumza katika jukwaa hilo, alimpongeza Rais John Magufuli kwa kuwajali wakulima na kuongeza kuwa amekuwa mtetezi wa wakulima dhidi ya dhuluma alipoagiza mzigo wa mazao chini ya tani moja usitozwe ushuru barabarani.

Mtutu ambaye ni mjumbe wa kamati ya siasa wilayani hapo, kupitia mkutano huo, alimwomba Rais Magufuli kuwatatulia tatizo sugu wakazi wa kata ya Kisiju kwa kuimalizia barabara ya lami kutoka Mkuranga hadi Kisiju.

Alimwomba pia kuwajengea gati katika bandari yao na kuirasimisha ili wanavijiji vya Kisiju Pwani, Koma, Kwale, Kuruti na Goza ambao uchumi wao unategemea Bahari ya Hindi wainuke kimaisha.

# TARI yawakumbusha wakulima kanuni za kilimo

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

KITUO cha Utafiti wa Kilimo Kanda ya Kusini cha TARI Uyole, kimewataka wakulima kuendelea kuzingatia kanuni bora za kilimo wanazoelekezwa na wataalamu, ikiwa ni pamoja na kutumia mbegu zilizofanyiwa utafiti na kuboreshwa, badala ya kulima kiholela.

Mkurugenzi wa kituo hicho, Dk. Tulole Bucheyeki, alitoa ushauri huo juzi alipotembelea mashamba ya wakulima katika Kijiji cha Ilunda wilayani Njombe na kuelezwa kufurahishwa na mwenendo wa wakulima.

Alisema maendeleo makubwa yanaonekana kwenye kazi zao ni baada ya kupewa elimu ya utaalamu wa kilimo pamoja na matumizi ya mbegu bora zinazofanyiwa utafiti na kituo cha utafiti cha Uyole.

"Hapa Ilunda nimefurahishwa, lakini kuna baadhi ya wakulima ambao hawatumii teknolojia ambazo tunawafundisha. Lakini tuna mbinu nyingi za kuendelea kufaulisha hizo teknolojia na tutaendelea kuwafundisha zaidi na zaidi," aliahidi Dk. Bucheyeki.

Nickson Mbogela, moja wa wakulima wa mahindi na viazi na mazao mengine aliyetembelewa katika kijiji cha Ilunda, akizungumza katika mahojiano, alisema ujuzi walioupata kupitia kituo cha utafiti kwenye mazao hayo umewasaidia kupata tija na kuwawezesha familia zao kukua kiuchumi.

"Ninalima mahindi na viazi, kwa kweli elimu imenisaidia sana kupata mazao bora na ninavuna mazao mengi yanayoniwezesha kupata chakula na nikiuza naweza kupeleka watoto shule bora. Nimejenga nyumba, lakini nimenunua ng'ombe na nguruwe," alisema Mbogela.

Milton Myava, mkulima wa maparachichi katika kijiji hicho alisema, kupitia mashamba darasa wamepata msaada mkubwa wa kulima na kuzalisha kwa tija, kwa kuwa ameboresha kilimo chake ikilinganishwa na hapo awali walipokuwa wanalima kwa mazoea.

"Tulikuwa hatujui kama maparachichi yatakuwa ni biashara au yatatupatia kipato, lakini ndani ya miaka mitatu mimi nilivuna na kwa kweli kupitia TARI nimeweza kugundua kuwa hili ni zao la biashara ambalo lipo vizuri hapa na pote duniani."

Ofisa Kilimo wa Kijiji cha Ilunda, Disbord Ntila, alisema wanaendelea kuwaelekeza wakulima namna ya kuzingatia kulima kitaalamu hatua ambayo imebadili maisha yao licha ya kuwapo kwa baadhi ya changamoto zikiwamo gharama kubwa za pembejeo pamoja na kukosekana kwa mtaji wa kutosha.

Nipashe
Spotika



WACHEZAJI 10 BORA WA EPL 2020 UK. 12-13

# REKODI 5 ZA RONALDO 2020



**TURIN,** Italia

JINA la Cristiano Ronaldo limejaa kwenye rekodi. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno ameufanya mchezo wa soka kuonekana rahisi huku akizivunja rekodi nyingi.

Mara zote ana njaa ya changamoto mpya, Ronaldo kwa sasa anang'ara kule kwenye Ligi Kuu Italia, Serie A, akiwa na Juventus na bado ni mchezaji bora licha ya umri wake wa miaka 35.

Ni vigumu kusema kwamba, umri wa Ronaldo umemkamata kutokana na uwezo wake dimbani. Kiukweli amepoteza kasi, lakini bado kiwango chake ni cha juu zaidi. Huamini katika hilo?

Hapa tunaangalia rekodi za Ronaldo alizozivunja kwa mwaka huu wa 2020 pekee.

### #5. Mchezaji wa kwanza kufunga mabao 50 Serie A, LaLiga na EPL

Baada ya kujiunga na Juventus, Cristiano Ronaldo aliulizwa kwenye mahojiano kama 'amemmisi' Lionel Messi.

Na jibu lake lilikuwa hili: "Hapana, pengine yeye ndiye amenimisi mimi. Nimecheza England, Hispania, Italia na Ureno, na kwenye timu ya taifa, wakati yeye akiwa bado Hispania. Pengine ananihitaji zaidi mimi. Kwa upande wangu mimi maisha ni changamoto, napenda hilo, na napenda kuwafanya watu wawe na furaha."

Na baada ya misimu miwili na nusu, ameshakamilisha kile alichokuwa anakitaka. Ni mchezaji muhimu kwa kocha Andrea Pirlo pale Juventus na amekuwa nguzo muhimu kwa kufunga mabao. Amekuwa mchezaji wa kwanza kufunga zaidi ya mabao 50 katika ligi kubwa tatu za Ulaya.

### #4. Kufikisha haraka mabao 50 Serie A

Ndiyo, wakati Cristiano Ronaldo alipofikisha umri wa miaka 33, kulikuwa na mjadala mkubwa kama angeweza kuwika kule Juventus kipindi aliposajiliwa kwa euro milioni 100.

Misimu kadhaa baadaye, Cristiano Ronaldo anaonyesha bila shaka yoyote kwamba, ni binadamu wa aina yake. Ni mashine ya kufunga mabao na Ronaldo amekuwa kwenye msimu bora zaidi.

Katika msimu wake wa kwanza, alifunga mabao 21 kwenye Serie A. akafuatia na mabao 31 katika mechi 33 msimu wa 2019-20 na amevunja rekodi ya kuwa mchezaji wa kwanza kufikisha kwa haraka mabao 50 kwenye Ligi Kuu Italia akiwa amefanya hivyo katika mechi 61 tu.

### #3. Mabao 30 kwa msimu mmoja

Wachezaji wengi huwa na furaha wanapofunga mabao 30 kwa msimu mmoja kwenye ligi. Ni jambo la kufurahisha ukifanya hivyo katika kiwango cha juu.

Alifanya hivyo kwenye Ligi Kuu England, LaLiga na sasa Serie A.

### #2. Mabao zaidi ya 10 misimu 16 mfululizo

Mwaka huu, Ronaldo amekuwa mchezaji wa kwanza kufunga mabao zaidi ya 10 kwa misimu 16 mfululizo. Ukiwa na Ronaldo katika kikosi chako maana yake ni kwamba una uhakika wa kupata mabao wakati wowote. Uzuri ni kwamba, tangu amejiunga na Juventus, amekuwa na kiwango kilekile cha kufunga.

Hii maana yake ni kwamba, amekuwa na kiwango mwendelezo wa kufunga mabao na kuwa mmoja wa wachezaji wachache zaidi duniani kufanya hivyo.

### #1. Kufunga mechi 11 mfululizo katika michuano mitatu tofauti

Nusu ya msimu wa 2019-20, Ronaldo alijiwekea rekodi ya aina yake kwenye kufunga mabao. Alifikia rekodi ya kufunga katika mechi 11 mfululizo kwenye Serie A iliyowekwa na Rui Costa na Gabriel Batistuta.

Pia alikuwa mchezaji wa kwanza kufunga mabao katika mechi 11 kwenye michuano mitatu tofauti. Alifunga katika mechi 11 mfululizo kwenye LaLiga, Ligi ya Mabingwa Ulaya na sasa Serie A.

Hiyo ni sawa na Jamie Vardy ambaye alifunga katika mechi 11 mfululizo kwenye Ligi Kuu England wakati Leicester ikitwaa taji la ligi hiyo.

## ISIKUPITE

HAKUNA mchezaji yeyote katika Ligi Kuu England aliyefunga bao la kwanza mara nyingi msimu huu zaidi ya straika wa Arsenal, Alexandre Lacazette, ambaye amefanya hivyo mara nne kwenye mechi sita za 'Gunners'.



Extra Time

# WACHEZAJI 10 BORA WA EPL 2020

**LONDON,** England

MWAKA wa aina yake unaelekea ukingoni, huku soka likiwa limeathiriwa kwa kiasi kikubwa na mlipuko wa virusi vya corona, na mechi zikichezwa bila mashabiki uwanjani, lakini Ligi Kuu England imebaki kuwa ndio inayovutia zaidi duniani.

**Liverpool waliutwaa ubingwa msimu uliopita, na msimu huu mambo yanaonekana kwenda vizuri kwa upande wao.**

Mpira wa miguu umeendelea kuwa tukio linalovuta hisia za wengi duniani, licha ya mlipuko wa virusi vya corona. Ligi Kuu England imewaibua wengi na kuwatoa wachezaji bora kabisa duniani.

Makala haya yanawaangalia wachezaji 10-bora kwenye Ligi Kuu England kwa mwaka 2020, na hii inatokana na viwango vyao dimbani...

### #10. JACK GREALISH, ASTON VILLA

Hata alipokuwa kwenye timu ya vijana, alichukuliwa kama mmoja wa wachezaji bora zaidi, na mwaka 2020 umemuimarisha zaidi Jack Grealish na kuwa mmoja wa wachezaji bora kwenye Ligi Kuu England.

Zao la akademi ya vijana ya Aston Villa, na kipaji cha Grealish hakina maswali. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 25, amekuwa nguzo ya Aston Villa na ndiye nahodha wa kikosi hicho.

Nyota huyo wa kimataifa wa England alikuwa akihusishwa zaidi na Manchester United kipindi cha majira ya joto na akasaini mkataba mpya kule Aston Villa. Ana uwezo wa kucheza winga zote, na atabaki kuwa mchezaji ambaye atakaa kwa muda mrefu zaidi pale Villa.

### #9. JORDAN HENDERSON, LIVERPOOL

Nahodha huyu wa Liverpool alikaribia kuondoka Liverpool kwenda kujiunga na Fulham.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 30, alijiunga na Liverpool kutoka Sunderland mwaka 2011 kwa ada ya pauni milioni 16, na msimu mmoja baadaye alikaribia kujiunga na Fulham. Hata hivyo, kiungo huyo alitulia na kupewa uongozi wa kurithi mikoba ya unahodha ya Steven Gerrard.

Henderson alikuwa mmoja wa wachezaji muhimu wa Liverpool walioshinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya misimu miwili iliyopita.

### #8. JAMIE VARDY, LEICESTER CITY

Kwa muda sasa imeshauriwa kwamba, Leicester City inatakiwa kuwekeza kwa washambuliaji vijana kwa ajili ya kuchukua nafasi ya Jamie Vardy katika siku za usoni, lakini uwezo wa straika huyo mbele ya goli ni wa kuvutia.

Klabu hiyo ilimnunua Islam Slimani na baadaye Kelechi Iheanacho ili kumpa ushindani Vardy, lakini wachezaji wote wameshindwa kuchukua nafasi yake. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, ameendelea kufunga mabao, akiiongoza Leicester City kuwa kwenye ubora kabisa.

Nyota huyo wa kimataifa wa England alitwaa tuzo ya Kiatu cha Dhahabu msimu uliopita baada ya kufunga mabao 23 katika mechi 35.

### #7. TRENT ALEXANDER-ARNOLD, LIVERPOOL

Bila shaka yoyote, kwa sasa ndio mlinzi bora wa kulia duniani, Trent Alexander-Arnold ameendelea kutoa mchango wake mkubwa kwa timu.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 22, ni zao la akademi ya Liverpool, tangu alipoanza kuichezea mwaka 2016. Chini ya uongozi wa Jurgen Klopp, Alexander-Arnold amekuwa bora zaidi, hasa kwa ubunifu wake na namna anavyocheza.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England amekuwa akicheza pamoja na mlinzi wa kushoto, Andrew Robertson na wamekuwa na msaada mkubwa kwa kikosi cha Liverpool katika kusaidia mashambulizi.

### #6. SADIO MANE, LIVERPOOL

Mmoja wa mawinga bora duniani kwa sasa, Sadio Mane amefurahia wakati mzuri zaidi pale Liverpool.

Mane alijiunga na Liverpool kutoka Southampton mwaka 2016 kwa ada ya pauni milioni 34, huku kocha, Jurgen Klopp akiwa shabiki wake tangu alipokuwa anainoa Borussia Dortmund. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, haraka akawa mchezaji muhimu kwa Liverpool.

Msimu uliopita, nyota huyo wa kimataifa wa Senegal alifunga mabao 18 kwenye mechi 35 za Ligi Kuu England wakati Liverpool wakitwaa taji la Ligi Kuu England na amekuwa kwenye kiwango bora msimu huu, akifunga mbao manne katika mechi 12.

### #5. BRUNO FERNANDES, MANCHESTER UNITED

Kila mpenda soka anajaribu kufikiria namna gani Manchester United wangekuwa kwenye wakati mgumu kama wasingemsajili, Bruno Fernandes, Januari mwaka huu.

Akiwa anahusishwa na 'Mashetani Wekundu' hao mara kadhaa, Fernandes alijiunga na Manchester United kutoka Sporting CP kwa pauni milioni 47 kipindi cha dirisha dogo la usajili. Amekuwa kwenye kiwango bora zaidi na kutwaa tuzo ya Sir Matt Busby kama mchezaji bora wa mwaka.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 26, kwa sasa anachukuliwa kama mchezaji muhimu zaidi wa Manchester United, akicheza kwa ubunifu wa hali ya juu kwa kuunganisha safu ya kiungo na ushambuliaji.

### #4. SON HEUNG-MIN, TOTTENHAM HOTSPUR

Pamoja na Mane na Mohamed Salah, Son Heung-Min ni miongoni mwa mawinga bora zaidi duniani kwa sasa.

Wakati Harry Kane akiendelea kuwa nyota wa Spurs, Son bila shaka yoyote ni mchezaji muhimu sana kwa kikosi hicho. Raia huyo wa Korea Kusini amekuwa na msimu wa kuvutia zaidi pale Spurs.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 28, ametengeneza upatina mzuri kati yake na Kane chini ya kocha, Jose Mourinho. Amefunga mabao 11 katika mechi 30 msimu uliopita, na tayari Son amefunga mabao 11 msimu huu katika mechi 13.

### #3. MOHAMED SALAH, LIVERPOOL

Liverpool ina wachezaji wengi bora duniani kwa sasa, na Mohamed Salah bila shaka yoyote yupo kwenye kiwango bora kabisa.

Uhamisho wake wa pauni milioni 38 kutoka Roma kwenda Liverpool mwaka 2017, umemfanya kuwa mmoja wa wachezaji bora zaidi akiwa pia alishawahi kuichezea Chelsea. Hata hivyo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, amekuwa nguzo imara zaidi kwa kocha, Jurgen Klopp, akifunga mabao 32 kwenye Ligi Kuu katika msimu wake wa kwanza.

Tangu hapo, Salah hajaangalia nyuma, ameendelea kufunga mabao katika kila mechi. Msimu uliopita alifunga mabao 19 katika mechi 34 wakati Liverpool iliposhinda taji la Ligi Kuu England. Msimu huu anaonekana kuwa kwenye nafasi nzuri ya kuivunja rekodi yake ya msimu uliopita kwani tayari ameshafunga mabao 11 katika mechi 12 msimu huu.

### #2. HARRY KANE, TOTTENHAM HOTSPUR

Kulikuwa na hofu chini ya utawala wa Mauricio Pochettino, kwamba kiwango cha Harry Kane kinaweza kudidimia kutokana na majeraha ya mara kwa mara.

Chini ya Mourinho, mchezaji huyo wa kimataifa wa England anaonekana kama amefufuka. Upatina wake na Son Heung-Min umekuwa muhimu zaidi kwa Spurs msimu huu, na wanaoneka kwamba wataendelea kuwa bora zaidi.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, amekuwa nguzo muhimu zaidi kwa sasa. Kane amefunga mabao tisa katika mechi 13 za Ligi Kuu msimu huu, lakini ametoa pasi za mwisho 10.

### #1. KEVIN DE BRUYNE, MANCHESTER CITY

Kevin De Bruyne alichaguliwa kuwa mchezaji bora wa mwaka wa Ligi Kuu msimu uliopita kutokana na kiwango chake bora kabisa, na alistahili tuzo hiyo.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji ni mmoja wa wachezaji bora zaidi pale Manchester City, huku ubunifu wake ukiwa nguzo muhimu kwa kikosi hicho cha kocha, Pep Guardiola. Msimu uliopita, alitengeneza pasi za mwisho 20, akiifikia rekodi ya Thierry Henry ya kuwa na pasi za mwisho nyingi zaidi kwa msimu mmoja.

Huku David Silva akiwa ameondoka kipindi cha majira ya joto kilichopita, kumekuwa na presha kubwa zaidi kwa nyota huyo mwenye umri wa miaka 29, kuendelea kuwa juu. De Bruyne amefanya makubwa hadi sasa; katika mechi 10 za Ligi Kuu alizoanza, raia huyo wa Ubelgiji ametoa pasi za mwisho sita na kufunga mabao mawili.



DE BRUYNE

## Nukuu

"Mungu amenifanya nicheze vizuri. Ndiyo maana kila wakati ninapotoka uwanjani hufanya ishara ya msalaba. Ninahisi nitakuwa nikimsaliti kama sitafanya hivyo, " **nguli wa soka wa zamani, Diego Maradona, enzi za uhai wake**



"Sitaki kufikiria kuhusu hatua hiyo (kuondoka) kwa sababu nitakuwa nafikiria kwa njia hasi na sitaki kufanya hivyo, kwa wakati huu, natakiwa kujaribu hatua chanya zaidi kadri ninavyoweza. Tunapitia kipindi kigumu, kitu cha mwisho tunachotakiwa kufikiri ni kwamba, matatizo yetu yote yatamalizika kwa miezi michache ijayo. Sitaki kufikiria kuhusu matatizo kwa sasa," **Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta**



"Kama wewe, najua namna gani unapenda kuvaa jezi ile ile kila siku, hongera sana kwa kuifikia rekodi hiyo katika historia yako ya soka, Lionel [Messi]. Lakini juu ya yote, hongeza kwa kipindi chako kizuri hapo Barcelona. Habari yako ni kama yangu, kuipenda klabu moja kwa muda mrefu, bahati mbaya kwa soka la kisasa ni nadra sana. Unanivutia sana,@leomessi," **Pele akimpongeza Messi kwa kufikia rekodi yake ya kufunga mabao 643 katika mechi 656 kwa klabu moja kama yeye alivyofanya akiichezea Santos kati ya mwaka 1956 na 1974.**






# MATUKIO 10 MAKUBWA YA MICHEZO YALIYOTIKISA 2020

**Na Adam Fungamwango**

MWAKA 2020 unayoyoma, na zimebaki siku tatu tu kuumaliza kwa mapenzi yake Mwenyezi Mungu. Ni mwaka uliokuwa na mambo mengi mno kiasi kwamba umeonekana mwaka mfupi zaidi kuliko miaka yote iliyopita.

**Ukiachilia mbali mambo ya uchaguzi nchini Tanzania, lakini janga la ugonjwa wa COVID-19, unaosababishwa na virusi vya corona am bao umeutikisa dunia, ulisababisha kuonekana kama dunia imesimama hivi.**

Nchi zingine watu walijifungia ndani. Hakukuwa na kitu kingine kilichokuwa kikiendelea. Nchini Tanzania ingawa hali haikuwa mbaya kihivyo kama wenzetu, lakini watu waliishi kwa tahadhari kubwa na kwa maelezo maalum kutoka kwa wataalamu wa afya.

Kwenye makala haya tuaangazia matukio yote ya kukumbukwa kwenye michezo yaliyotokea nchini Tanzania kwa mwaka mzima wa 2020 uliosalia siku nne tu kumalizika...

### #1. Corona kusimamisha michezo yote

Serikali ilisimamisha michezo yote ikiwamo Ligi Kuu Tanzania Bara katikati ya mwezi Machi kutokana na kuibuka kwa ugonjwa wa COVID-19, unaosababishwa na virusi vya corona.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alitangaza kusimamisha shughuli zote za michezo yote kama Ligi Kuu na zingine za chini yake, michezo ya shule za msingi, sekondari na mashirika ya umma ambayo hufanyika kila mwaka, yote ilisitishwa kutokana na ugonjwa huo kuanza kugundulika kwa baadhi ya wagonjwa nchini. Na hatua hiyo ilichukuliwa ili ugonjwa usisambae zaidi.

### #2. Rais Magufuli kuruhusu michezo yote

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, pamoja na mambo mengine, aliruhusu tena michezo kuanza Juni Mosi, baada ya kusimama kwa takribani miezi miwili hii ikitokana na kupungua kwa kasi ya maambukizo ya ugonjwa wa COVID-19 unaosababishwa na virusi vya corona hapa nchini.

Rais alitangaza ruhusa hiyo mwezi Mei na ilipofika Juni Mosi, vyama na michezo vikaanza kuweka utaratibu wa jinsi ya kuanza tena michezo na mambo yakaendelea kama kawaida.

### #3. Simba kutwaa ubingwa mara tatu mfululizo

Ilikuwa ni Juni 28, mwaka huu, klabu ya Simba ilipofanikiwa kutwaa ubingwa mara ya tatu mfululizo baada ya sare ya bila kufungana dhidi ya Tanzania Prisons kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya.

Kutokana na sare hiyo, Simba ikajikusanyia pointi 79 ambazo hazikuweza kufikiwa na timu yoyote, ikiwa imebakiwa na mechi sita mkononi.

Mara ya mwisho Simba kutwaa ubingwa zaidi ya mara mbili ilikuwa ni mwaka 1976 hadi 1980, ilipotwaa mara tano mfululizo. Baada ya hapo ikizidi ilikuwa ikitwaa mara mbili mfululizo. Mara ya mwisho ilikuwa ni msimu wa 2003 na 2004.

Simba imetwaa ubingwa mara tatu mfululizo baada ya kufanya hivyo kuanzia msimu wa 2017/18, 2018/19 na 2019/20.

### #4. Morrison kushinda kesi na kujiunga na Simba

Moja kati ya matukio yaliyosumbua vichwa vya mashabiki wa soka nchini ni sakata la mchezaji Benard Morrison Agosti mwaka huu. Wakati huo akiwa na Yanga, alifungua kesi ya kimkataba dhidi ya waajiri wake, Yanga.

Ni tukio lililosababisha wanachama na mashabiki wa klabu za Simba na Yanga kushinda kwenye ofisi za Shirikisho la Soka nchini (TFF), kwa siku tatu hivi. Ni sakata lililochukua takriban wiki nzima. Siku moja kabla ya hukumu yake kutolewa, ukurasa rasmi wa klabu ya Simba ulitoa picha yake kuwa imemsajili akiwa kama mchezaji huru.

Kesho yake Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji Tanzania chini ya Mwenyekiti wake, Elias Mwanjala, alitangaza rasmi kuwa mchezaji huyo machachari ameshinda keshi yake kuhusu mkataba wake dhidi ya timu yake ya Yanga, hivyo yuko huru kujiunga na klabu yoyote.

### #5. Yanga kusajili wachezaji wawili kutoka AS Vita

Katika usajili ulioshtua wengi nchini Tanzania ni pale klabu ya Yanga ilipofanikiwa kuwanasa wachezaji wawili maarufu wa klabu ya AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo, Mukoko Tonombe na Tuisila Kisinda.

Usajili huo uliofanyika katikati ya Agosti, licha ya kuwashangaza na kuwashtua wanamichezo wengi nchini, lakini uliwafurahisha mno wanachama na mashabiki wa Yanga ambao waliandamana na kujazana Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere kuwapokea, kwani hawakutarajia kwa klabu yao jinsi ilivyokuwa kwa wakati huo ingeweza kumudu kuwasajili wachezaji hao mahiri.

### #6. Yanga kutimua makocha wawili

Agosti na Oktoba, klabu ya Yanga iliwatimua makocha wake wawili kwa sababu mbalimbali tofauti, ikiwamo pia timu hiyo kutokuwa na mwenendo wa kuridhisha kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mbelgiji Luc Eymael alitimuliwa Agosti mwaka huu, ambapo pamoja na mambo mengine, lakini kutoa maneno ya kibaguzi kwa wanachama na mashabiki wa klabu hiyo na Watanzania kwa ujumla.

Oktoba, kocha aliyechukua nafasi yake Mserbia Zlatko Krmpotic naye alitimuliwa kutokana na kile kilichoelezwa timu kutocheza soka la kuvutia, licha ya kwamba kocha huyo alikuwa hajafungwa mechi yoyote, lakini akipata ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Coastal Union.

### #7. Kiduku kumkong'ota Mthailand

Ilikuwa ni mwanzoni tu mwa Novemba wakati bondia anayekuja juu kwa kasi nchini, Twaha Kiduku alipomkong'ota bondia kutoka nchini Thailand, Sorimongkhon Singwancha kwa TKO.

Twaha alimzimisha bondia huyo kwenye raundi ya saba akasalimu amri.

### #8. Mwakinyo kumfumua Muargentina

Bondia mashuhuri nchini, Hassan Mwakinyo, alidhihirisha ubabe wake, alipomtwanga bondia Jose Carlos Paze kwa TKO kwenye raundi ya nne tu, katika pambano lililokuwa la raundi ya 12.

Pambano hilo lilifanyika Novemba, mwaka huu kwenye Ukumbi wa Next Door Arena maeneo ya Masasani jijini Dar es Salaam na kubeba mkanda wa WBF.

### #9. Simba kushinda mechi ugenini, Nigeria

Mwishoni mwa Novemba, kwa mara ya kwanza kwenye historia ya soka la Tanzania, klabu kutoka nchini ilipata ushindi ikiwa ardhi ya Nigeria.

Timu ya Simba iliifunga Plateau United bao 1-0 kwenye Mji wa Jos, uliopo Abuja nchini Nigeria na kuwa timu ya kwanza ya Tanzania kushinda nchini humo.

Hakuna timu yoyote ile ya Tanzania iliyowahi kushinda nchini humo huko nyuma ikiwamo Simba yenyewe ambayo ilicheza na timu mbalimbali kama Racca Rovers, Enyimba.

### #10. Timu za vijana U-20, U-17 kufuzu AFCON

Moja kati ya matukio ya kukumbukwa kwa mwaka huu ni Tanzania kufanikiwa kuingiza timu mbili za vijana kwenye fainali za michuano ya Afrika, AFCON chini ya miaka 20 na 17.

Timu ya vijana chini ya miaka 20, mwishoni mwa Novemba ilifuzu AFCON kwa kuichapa Sudan Kusini bao 1-0 kwenye michuano ya CECAFA iliyofanyika nchini Tanzania, Karatu mkoani Arusha kwenye mechi ya nusu fainali, ingawa timu hiyo ya Ngorongoro Heroes ilichapwa mabao 4-1 dhidi ya Uganda kwenye mechi ya fainali.

Mwezi huu wa Desemba, timu ya vijana chini ya miaka 17, Serengeti Boys nayo ilifuzu AFCON itakayochezwa mwakani nchini Morocco, baada ya kuichapa timu ya taifa ya Ethiopia kwa mikwaju 4-3 ya penalti baada ya sare ya bao 1-1 kwa dakika 90, kwenye mchezo wa nusu fainali uliochezwa Uwanja wa Umuganda mjini Rubavu nchini Rwanda, ikiwa ni ni michuano ya CECAFA, Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati ambapo pia hutumika kutafuta timu za kuwakilisha AFCON kwa ukanda husika. Hata hivyo, timu hiyo ilifungwa mabao 3-1 dhidi ya Uganda kwenye mechi ya fainali.

**JE, WAJUA?**



MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Edinson Cavani, amehusika katika mabao matano akitokea benchi msimu huu (akifunga matatu na pasi mbili za mwisho), ambazo ni mbili zaidi kuliko mchezaji yeyote kwenye ligi hiyo.



# ‘Walimu katumieni mbinu mlizofunzwa’

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

CHAMA cha Walimu Tanzania (CWT), kimewataka walimu kuzitumia kwa vitendo mbinu za ufundishaji elimu ya awali kwa wanafunzi wao ili kukuza kiwango cha taaluma.

Katibu wa CWT, Deus Seif, alisema hayo katika mahafali ya walimu ya kuhitimu mafunzo ya astashahada (diploma ya masomo ya awali ) ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania yaliyofanyika hivi karibuni jijini hapa.

Katika mahafali hayo walimu 436 kutoka Wilaya ya Chemba na Mpwapwa walihitimu masomo hayo ambayo yanaelezwa kuwa ni muhimu kwa sababu ndiyo msingi wa mwanafunzi kabla ya kuendelea na ngazi au hatua zinazofuata.

Katibu Seif alisema wakitumia mbinu hizo kwa vitendo katika shule wanazofundisha, itakuwa rahisi kuwasaidia wanafunzi kuelewa kwa haraka wanapokuwa darasani.

“Alisema wamekuwa walimu wa kwanza katika Wilaya za Chemba na Mpwapwa kupata elimu hiyo, chini ya mradi wa majaribio unaoendeshwa na Vyama vya Walimu Duniani kwa kushirikiana, CWT na serikali hivyo wanapaswa kuonyesha bidii katika ufundishaji ili Dodoma iwe mfano wa kuigwa kielimu.

Katibu huyo alisema, CWT imefanya kazi kubwa ya kuhakikisha walimu wake wanapata nafasi hiyo, hivyo nao wanapaswa kuonyesha uwezo mkubwa wa kutoa taaluma hiyo kwa wanafunzi.

Mwenyekiti wa mradi huo, Aboubakary Allawi, aliishukuru serikali pamoja na maofisa elimu wa mkoa na wilaya hizo kwa kukubali kuwaruhusu walimu kwenda kusoma ili kuongeza taaluma ya ufundishaji.

Alisema mradi huo wa majaribio ulianza rasmi 2017 na kwamba jumla ya walimu 500, kutoka wilaya ya Chemba na Mpwapwa walidahiliwa kupitia vigezo vya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kujiunga na masomo hayo.

Alisema mafunzo haya yanastahili kupewa umuhimu sana kwa walimu kwa sababu yatakuwa chachu ya maendeleo kwa walimu kutokana na wengi wao kushawishika kujiendeleza kitaaluma.

“Tunawashukuru sana wadau wa elimu kwa kukubali mradi huu ufanyike, tunaamini unakwenda kuleta matokeo chanya kwa walimu na wanafunzi,” alisema Allawi. Aliongeza kuwa lengo lao ni kuona walimu wanakwenda na wakati katika ufundishaji ndiyo maana wameamua kuanzisha mradi huo wa elimu ambao unatoa hamasa kwa walimu kujiendeleza kimasomo.

Kutokana na hilo alisema walimu wanapaswa kuchangamkia fursa kama hizo zinapotokea ili kuhakikisha wanakuza viwango vyao vya elimu.

Aliishukuru CWT kutokana na kuchangia kwa asilimia 100 kuhakikisha walimu hao wanahitimu masomo yao.



Wafanyakazi wa kampuni ya ujenzi ya Hainan wakijaza kifusi sehemu ambazo zimeharibika, katika barabara ya Goba Tegeta A, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wauza matunda masoko hatarishi ‘wapigwa stop’

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imepiga marufuku wafanyabiashara wa matunda, kushusha mizigo nje ya masoko kutokana na sehemu hizo kutokuwa salama kiafya.

Marufuku hiyo ilitolewa na jiji hivi karibuni kutokana na maeneo ambayo wafanyabiashara hao kuyatumia kushusha matunda kuwa kuhatarisha kwa afya za walaji.

Zaidi ya wafanyabiashara 58, waliokuwa wakileta na kushusha matunda yakiwamo mananasi na matikiti maji nje ya eneo la soko la Sabasaba wamezuiliwa kufanya hivi kuanzia sasa.

Kutokana na agizo hilo la Ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji wafanyabiashara hao wamemwomba Mkurugenzi wa Jiji kushirikiana nao kutafuta eneo mbadala litakalotumika katika biashara hiyo. Ofisa Masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna, akifafanua kwa waandishi wa habari kuhusiana na kusitisha eneo hilo kushusha na kuuza matunda, alisema kuwa siyo rasmi bali wafanyabiashara hao walivamia na kukiuka utaratibu na miongozo kwa mujibu sheria.

“Maeneo bado tunayo ya kutosha kwa ajili ya kushushia mizingo likiwamo la soko la Ndugai, Bonanza na sehemu nyingine ambazo wanaweza kushusha kulingana na mizigo husika, siyo hapa ambako wamejiamulia wenyewe,” alisema.

Naibu Meya wa Jiji la Dodoma, Emmanuel Chibago, akizungumza na wafanyabiashara hao alisema eneo hilo haliko rasmi kushushia na kuuza matunda hayo, wafanyabiashara hao wanaoleta matunda hayo wanatakiwa kuheshimu misingi, sheria na utaratibu ambao unaozuiliwa kufanya biashara maeneo yasiyo rasmi. Mfanyabiashara Denis Athumani, akizungumza na waandishi wa habari kuhusu hatua hiyo, alisema wanaiomba Ofisi ya Mkurugenzi kuwashirikisha kusaka eneo jingine ili kupata sehemu itakayokuwa rafiki kwa biashara hiyo ya matunda.

“Tupo tayari kuondoka maeneo yote yanayovamiwa, lakini kilio chetu kikubwa ni halmashauri ya jiji inapotutaka kupisha sehemu hizo, kama hii ililopo nje ya soko la Sabasaba, tunaomba tushirikishwe huko tunakopelekwa katika kuweka mazingira kwa upande wa miundombinu kulingana na biashara zenyewe zilivyo,” alisema Athumani.

Athumani, alisema analipongeza jiji hilo kwa kuhakikisha maeneo yake yanakuwa kwenye mazingira safi.

“Wamekuwa wakitoa elimu kwanza kabla ya wafanyabishara kuondolewa, hii imesababisha maana halisi ya ushirikiano kati yetu na wafanyabiashara na kuwezesha kuwaondolea chuki na kujenga mahusiano mazuri na Ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji,” alisema.

# Wahimizwa kulifanya jiji lao kuwa la kijani

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAKAZI wa Dodoma wametakiwa kupanda miti kwa wingi kipindi hicho cha mvua za masika, ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi pamoja na kuhifadhi mazingira.

Mwenyekiti wa kikundi cha uhifadhi na utunzaji mazingira cha Chapakazi cha jijini hapa, Khalid Hamadi, alisema, wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Hamadi aliwaomba wakazi wa mkoa wa Dodoma, kupanda miti kulingana na aina ya ardhi wakati huu wa msimu wa mvua ili kuhifadhi na kutunza mazingira.

Alisema ardhi ya Dodoma inatofautiana hivyo, kuna aina ya miti ya kupanda kulingana na eneo husika hasa miti ya matunda ili iweze kuota, kutoa matunda na kuendelea kustawi.

Aidha, aliwaomba wakazi hao kupata ushauri wa aina gani ya mti ambao wanahitaji kupanda kwenye eneo husika ili iweze kufanikiwa malengo ya kuufanya mkoa huu kuwa wa kijani.

“Sisi wenyewe pia tumekuwa wataalamu ambao tunaoweza kutoa ushauri na tutakuwa tayari kushauri kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizoelekezwa juu ya mazingira,” alisema.

“Ushauri huu hata pia kwenye upande wa mti unavyopandwa, na aina za mbolea ya kuweka, jinsi ya kupanda garden msimu huu wa mvua kwani kuna aina tofauti tofauti za majani (ukoka) ambao unatakiwa kupandwa kulinga na aina ya udongo ambao upo katika eneno husika,” alisema.

Mwenyekiti huyo wa kikundi hicho aliwataka wakazi wa Dodoma kufika katika ofisi zao ili wajionee jinsi ambavyo wanazalisha vungu vingi vya mapambo ambavyo hutumika katika maeneo mbalimbali.

“Sasa hivi tuna vyungu vya kuweka ofisini, harusini na majumbani, lakini tunatengeneza zawadi za kila aina kwa ajili ya maharusi, sikukuu za kuzaliwa na jinsi ambavyo atataka mteja wetu,” alisema.

Aidha, aliwataka vijana wenzake kutolalamika kwamba hakuna ajira na badala yake wanatakiwa kufanya kazi kwa bidii ili kujiingizia kipato bila ya kuchagua aina ya kazi.

“Tumepewa eneo lingine na Dodoma kwa ajili ya kulitunza sababu kubwa ni viongozi wameona jinsi ambavyo tunaifanya Dodoma inakuwa ya kijani, kikubwa ni kufanya kazi fursa zitakuja,” alisema.



Mbunge wa Jimbo la Momba, Condester Sichalwe, akitoa ufafanuzi baadhi ya changamoto za barabara kwa wananchi wa Kata ya Ndalambo, Halmashauri ya Momba, mkoani Songwe juzi. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Wajenga shule maalumu waliopata 'four', ziro

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKOA wa Mbeya umeanza kujenga shule maalumu za sekondari katika kila halmashauri ambazo zitakuwa zinapokea wanafunzi wanaofeli kidato cha nne na kupata daraja la nne na sifuri.

Albert Chalamila, Mkuu wa Mkoa huo, alisema shule hizo zitapokea wanafunzi wanaopata madaraja ya nne na ziro kwenye mitihani ya kidato cha nne ili wairudie na itakuwa na madarasa mawili ya kidato cha tatu na nne.

Alisema zitakuwa mali ya serikali na kutumika kama mbadala wa vituo vya watu binafsi vya wanafunzi kurudia mitihani na watakaokuwa wanasoma watalipa ada kama ilivyo kwenye vituo vya binafsi.

Akizungumza na wanahabari mwishoni mwa wiki, Chalamila alisema utekelezaji wa wazo hilo, umeanza katika Jiji la Mbeya ambako inajengwa kwenye viwanja vipya vya Iziwa.

"Halmashauri nyingine zimeshaweka kwenye bajeti zake za mapato ya ndani kwa ajili ya kutekeleza agizo hilo. Hizi shule ni muhimu sana maana kundi la wanafunzi hao ni kubwa na hii itakuwa lazima," alisema Chalamila.

Aliongeza kuwa kitendo cha wanafunzi hao wanaofeli mitihani hiyo kutofuatiliwa ni hatari kwa kuwa wanaweza kuwa sehemu ya wahalifu wanaoleta shida mitaani.

Alisema walimu watakaokuwa wanafundisha shule hizo watakuwa ni wa serikali ambao wataajiriwa kwenye mfumo rasmi wa ajira lengo ni kutaka mkoa huo kuwa wa mfano kitaifa kwa ubunifu wa masuala ya taaluma.

Alisema lengo lake ni kutaka baadaye serikali kuu ishirikishwe ili ikiwezekana shule za mfumo huo zianzishwe nchi nzima kwa ajili ya kulihudumia kundi hilo linalofeli kadato cha nne.

Katika hatua nyingine, Chalamila alisema kwa sasa wanahimiza zaidi ujenzi wa shule za msingi zenye mchepuo wa Kiingereza ambao umeanzia jijini Mbeya na baadaye zitasambaa katika wilaya zote.

Alisema mpaka sasa jiji hilo lina shule tatu ambazo ni Benjamin Mkapa, Azimio na John Magufuli na kwamba mwakani nyingine mpya zitafunguliwa Uyole na Iwambi.

"Kutokana na uhaba wa maeneo tunasisitiza sana shule hizi zijengwe kwa mtindo wa ghorofa ili ardhi ndogo inayopatikana itosheleze mahitaji," alisema Chalamila. Pamoja na kwamba sasa hivi serikali inatekeleza sera ya elimu bila malipo, lakini kuna tatizo lingine limezaliwa ambalo ni idadi kubwa ya wanafunzi wanaofeli mitihani ya kidato cha nne inaongezeka, hivyo ubunifu unahitajika kukabiliana na tatizo hilo.

# TARI kutafiti alizeti, chikichi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

KUTOKANA na kuadimika kwa mafuta ya kupikia na kusababisha bei kupanda, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) kituo cha Uyole Mbeya, imeanza utafiti wa mbegu za mazao mbalimbali zinazotumika kuzalisha mafuta.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mkurugenzi wa kituo hicho, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema lengo ni kuongeza uzalishaji wa mazao hayo nchini utakaosaidia kuongeza uzalishaji wa mafuta na kupunguza bei za bidhaa hiyo.

Alisema mazao wanayalengwa zaidi ni alizeti na michikichi ambayo ndiyo yanayostawi zaidi katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na kwamba michikichi inalimwa zaidi katika Wilaya ya Kyela.

Dk. Bucheyeki alisema hakuna sababu ya bei ya mafuta kupanda kiasi hicho wakati mazao yanayotoa mafuta yanastawi vizuri kwenye maeneo mengi nchini.

"Tumeshaanza kulifanyia kazi tatizo hilo kwa kufanya utafiti na kuzalisha mbegu bora za mazao yanayozalisha mafuta, tutazalisha mbegu za alizeti za kutosha kwa ajili ya kuzisambaza kwa wananchi, lakini michikichi imeshaanza kusambazwa katika baadhi ya mikoa," alisema Bucheyeki.

Aliwataka wananchi kuchangamkia kilimo cha mazao hayo ambayo alidai yana soko kubwa na hayahitaji huduma kubwa kama ilivyo kwenye mazao mengine.

# Wananchi walia TARURA kuharibu 'daraja la mungu'

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

WAKAZI wa Kata ya Izumbwe katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wamelalamikia Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA), kupitisha barabara ya Swaya-Igale, juu ya daraja la asili maarufu 'daraja la mungu' lililopo kwenye Mto Mbalizi, wakidai kufanya hivyo ni kuharibu kivutio watalii hicho.

Walisema barabara hiyo ya Swaya-Igale inajengwa kwa kiwango cha lami, na kudai wana wasiwasi kuwa daraja hilo linaweza kuharibika endapo yatapita magari yenye uzito mkubwa na kuondoa historia ya eneo lao.

Walitoa malalamiko hayo juzi wakati wa ziara ya Mbunge wa Mbeya Vijijini, Oran Njeza, aliyetembelea kata hiyo kukagua maendeleo ya ujenzi wa barabara hiyo.

Oscar Asher, akizungumzia daraja hilo, alisema waliamini kuwa wakati wa usanifu wa barabara TARURA, ingepitisha daraja hilo sehemu nyingine ili lile la asili libaki kama kivutio utalii.

Walisema walishangaa wataalamu hao walipoanza ujenzi kupitisha daraja la kisasa juu ya la asili hali inayoharibu mandhari ya ya eneo hilo ambalo lingekuwa miongoni mwa vyanzo vya mapato ya vijiji.

"Hatujui hawa wataalamu wana uhakika gani kwamba hilo daraja litakuwa na uwezo wa kuhimili kubeba magari yenye uzito mkubwa, wasiwasi wetu ni kwamba linaweza likabomoka na kuleta madhara," alisema Asher.

Halikadhalika aliishukuru serikali kwa kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami kwa maelezo kuwa itawasaidia kurahisisha usafiri na usafirishaji wa bidhaa kutoka mashambani kwenda Mbeya Mjini kwenye masoko.

Akijibu, malalamiko ya wananchi hao, Meneja wa TARURA wa Wilaya ya Mbeya, Seleman Mzirai, alisema barabara hiyo yenye urefu wa kilomita tisa ujenzi wake umefikia asilimia 40.

Alisema kwenye usanifu wa barabara hiyo waliamua baadhi ya maeneo waweke zege ili kuiimarisha zaidi ikiwamo eneo la daraja hilo ambalo wananchi wanalalamikia kuwa linaweza likabomoka, lakini akiwahakikishia kuwa wataacha maji yaendelea kupita kama ilivyokuwa.

"Lakini kwenye hili daraja magari yatakayoruhusiwa kupita ni yale yenye uzito usiozidi tani 10, huu ndio uzito ambao hauwezi kuleta madhara kwenye daraja hili, hivyo wananchi msiwe na wasiwasi," alisema Mziray.

Aliwaambia kuwa barabara hiyo pamoja na daraja hilo la Mto Mbalizi linagharimu Sh. bilioni saba na linatarajiwa kukamilika Machi mwakani.

Alisema awali mradi huo ulitakiwa ukamilike mwezi huu (Desemba), lakini waliamwongeza mkandarasi muda kutokana na usanifu kufanyika upya baada ya ule wa awali kubainika kuwa hautafaa.

Akizungumza na wananchi wa kata hiyo, Mbunge Njeza, aliwataka kuitunza miundombinu yao kwa kuwa wanaofaidika ni wao wenyewe.

"Msije mkawa mnasema hii barabara imejengwa hapa basi ni ya TARURA hapana, hawa ni wakala wetu kwahiyo mwenyekiti wa kijiji na wananchi wako ninyi ndiyo mnatakiwa kuilinda," alisema Njeza.

Njeza alisema ataendelea kufuatilia ujenzi wa barabara hiyo pamoja na miradi mingine, ili kuhakikisha inakamilika kwa wakati na wananchi wanaanza kunufaika nayo.



# Maalim Seif aagiza majengo Mji Mkongwe kufanyiwa tathmini

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad, ameutaka uongozi wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja kushirikiana na Mamlaka ya Mji Mkongwe kufanya tathmini ya majengo yote yaliyokuwapo katika mji huo, ili kunusuru maisha ya watu wengine.

Aliyasema hayo baada ya kuwatembelea majeruhi waliopata ajali ya kufukiwa na kifusi baada ya jengo la Bait-El-Ajaib kuanguka Desemba 25.

Alisema, majengo mengi ya Mji Mkongwe ni ya zamani na yapo katika hali mbaya kutokana na ubora wake na tofauti na majengo ya sasa kutokana na kutokarabatiwa kwa muda mrefu.

"Mkuu wa mkoa ni vizuri mkae pamoja na Mamlaka ya Mji Mkongwe, mfanye tathmini, mpitie jumba moja baada ya jingine kuona kwamba linafaa kukaliwa na litalobainika halifai basi kusiwe na muhali katika kuwahamisha wananchi kwani maisha ya mtu ni muhimu sana," alisema. Makamu Seif alisema lengo la serikali ni kunusuru maisha ya wananchi, huku akibainisha kwamba maisha yao ni muhimu kuliko kitu kingine chochote.

Katika hatua nyingine Maalim Seif aliwapongeza askari wa vikosi vya SMZ, Jeshi la Polisi na JWTZ kwa kufanya kazi ya mfano ya kujitolea baada ya ajali hiyo na kufanikiwa kuwaokoa majeruhi wanne ambao wanaendelea na matibabu katika Hospitali Kuu ya Rufani Mnazimmoja.

Alisema, serikali itaendelea kushirikiana na vikosi vyake kuwaongezea uwezo wa kukabiliana na mafaa yatakapotokea, ikiwamo vitendea kazi, ili vikosi hivyo vifanye kazi kwa urahisi na kunusuru maisha ya watu.

Alipongeza hatua ya Serikali ya Oman kuendelea kushirikia na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kulifanyia ukarabati jengo hilo ili lirudi katika hali yake.

Naye Kamishna wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi Zanzibar, Ali Abdalla, alisema vikosi vinaendelea na shughuli za uokozi kwa kutoa kifusi na vifaa vingine katika eneo hilo na kuiomba serikali kuyaangalia majengo ya muda mrefu.

Hata hivyo, alisema katika kipindi hiki cha mvua wameshazungumza na wajenzi kuliziba kwa maturubali ili lisiweze kupata maji. Kwa upande wake daktari anayewahudumia majeruhi hao katika wodi ya mifupa Hospitali ya Mnazimmoja, Riffat Khalfan, alisema wamepokea majeruhi hao juzi Desemba 25 na kuwapatia huduma ya kwanza.

Alisema, kati ya wagonjwa wawili wapo katika chumba cha uangalizi maalumu (ICU) na wawili wapo katika wodi za kawaida.

Aliwataja wagonjwa waliolazwa ICU kuwa ni Haji Juma Machano (37), mkazi wa Chumbuni na Dhamir Salum Dhamir (37), mkaazi wa Kinuni ambao hali zao bado mbaya na madaktari wanaendelea kuchukua jitihada, ili kuhakikisha wananusuru maisha yao.

Kwa upande wao majeruhi Hamad Matar Abdalla alisema, hali yake inaendelea vizuri pamoja na kupata majeraha ya mbavu na mkono, yaliyosababisha kukatwa kwa vidole vitatu na kuvunjika bega la upande wa kushoto.

Naye Majeruhi Ali Ramadhan Juma, alisema hali yake inaendelea vizuri na alipofikishwa katika hospitali alikuwa hajifahamu, lakini tayari hivi sasa anapata kumbukumbu.

Waliipongeza serikali kupitia Wizara ya Afya kwa kupatiwa huduma na hali yake inaendelea vizuri.

Haji Chum Khamis, mmoja wa ndugu wa marehemu Buruhani Ali Mavuno, alisema, wamepokea kwa masikitiko makubwa msiba wa ndugu yao ambaye ameacha mke na watoto wawili.



Katibu wa Ushirika wa Vijana wenye Taaluma Zanzibar (UVITAZ), Hakimu Omar Kulukulu, akizungumza na watumiaji wa dawa za kujiunga na kliniki ya Methadol iliyopo Kidongo Chekundu, ili kupata matibabu ya kuweza kuachana na dawa hizo, Jumbi kwa Mapwenti Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# UVITAZ yawataka waathirika dawa za kulevya kwenda kliniki

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

BARAZA la Vijana Zanzibar likishirikiana na Ushirika wa Vijana wenye Taaluma Zanzibar (UVITAZ), limewataka vijana wanaotumia dawa za kulevya kujiunga na kliniki ya Methadone, Kidongo Chekundu ili kupata tiba na kuondokana na majanga hayo.

Mwenyekiti wa Baraza la Vijana Zanzibar, Khamis Rashid Kheir, alisema hayo wakati wa ziara ya kutembelea vijiwe vya waathirika wa dawa za kulevya katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Aliwataka vijana walioathirika na dawa za kulevya wajiunge na kituo cha Kidongo Chekundu ili watumie dawa zitakazowasaidia kupunguza na kuondoa hamu ya uvutaji wa dawa hizo.

Alisema waathirika wa dawa hizo (waraibu) wana nafasi kubwa ya kuleta maendeleo ya nchi na kwamba ipo haja kujiweka tayari kuachana nazo ili kufanya kazi na kujipatia kipato halali.

"Waraibu wana nafasi ya kujitoa katika janga hili kwani zipo fursa nyingi za kupeleka maisha yao mbele kwa kujinasua na matumizi ya dawa," alisema.

Alisema ingawa kuna changamoto nyingi zinazowakabili waathirika hao, lakini Baraza la Vijana Zanzibar lipo tayari kuwasaidia kwa njia moja au nyingine ili kuhakikisha vijana hao wanaachana na uraibu huo pamoja na kujiunga katika Ushirika wa UVITAZ.

Katibu wa UVITAZ, Hakimu Omar Kulukulu, alisema shirika hilo lipo tayari kuhamasisha vijana walioathirika ili kujitoa katika janga hilo na kupeleka mbele gurudumu la maisha yao.

Alisema shirika linatoa elimu kwa waathirika wa dawa hizo pamoja na kuwapa nafasi ya kuwaendeleza kwa wale wenye vipaji kwa kuvitumia vipaji hivyo.

Aliwataka watumiaji hao kufanya uamuzi wa kuacha dawa hizo ili kuepukana na athari zake, ikiwamo wizi wa mali za watu na kuishi maisha hatarishi.

Naye mmoja wa wanachama wa UVITAZ, Mayunga Shaaban, ambaye alikuwa mwathirika wa dawa za kulevya, alisema hawana elimu ya kutosha kuhusiana na uwachaji wa dawa za kulevya na kuwataka kujiunga na kliniki hiyo ili kujitoa katika janga hilo.

Pia, waathirika hao walisema wapo tayari kuachana na dawa hizo na kwamba wamepoteza uaminifu katika jamii na maisha yao kuwa katika hatari.

# Ataka orodha waliohusika kupokea mil. 25/- za mwekezaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Wilaya ya Kaskazini 'B', Rajab Ali Rajab, amemwagiza Sheha wa Shehia ya Kiombamvua kuwasilisha orodha ya majina ya kamati iliyohusika na upokeaji wa fedha zaidi ya Sh. milioni 25 kutoka kwa mwekezaji wa kampuni ya Sea Rock Resort Limited, ambazo zilitolewa na mwekezaji kwa ajili ya utekelezaji wa makubaliano na wananchi wa shehia hiyo.

Alisema kwa mujibu wa maelezo aliyoyapata kutoka kwa wananchi fedha hizo zilipokelewa na kamati ambayo haikuwapo wakati wa kuingia makubaliano na kampuni hiyo na kamati halali ilizikataa fedha hizo baada ya kugundua kuwa haziendani na makubaliano ya awali.

Akizungumza na wananchi pamoja na uongozi wa kampuni huyo huko Nanjale, Shehia ya Kiombamvua kwa lengo la kusikiliza mgogoro kati ya mwekezaji na wananchi, Mkuu wa Wilaya alisema ni vyema wananchi wakaacha tabia ya kujihusisha na tabia ya kupokea fedha ambazo haziwahusu ili kuondoa migogoro kwa wananchi na wawekezaji.

Hata hivyo, kampuni hiyo imetakiwa kulipa stahiki za wafanyakazi ambao kwa muda mrefu hawajalipwa pamoja na kuahidi kufanya uhakiki wa wafanyakazi wazawa katika kampuni hiyo na kuangalia utekelezaji wa sheria ya utumishi kwa sekta binafsi.

Wakiwasilisha malalamiko hayo mbele ya Mkuu wa Wilaya, baadhi ya wananchi walisema eneo hilo la Nanjale wamelitumia kwa kipindi cha miaka sita wakiwa wanafanya shughuli za uvuvi ndio alipojitokeza mwekezaji huyo kwa madai ya kuwa amelinunua eneo hilo kwa ajili ya mwekezaji wa hoteli.

Hata hivyo, wananchi hao walisema waliingia mkataba na kampuni hiyo kwa makubaliano ya kupewa gari kwa ajili ya kusafirisha dagaa kutoka ufukweni mwa bahari hadi katika eneo walilokubaliana, ajira kwa wananchi.

Akitoa ufafanuzi, Ofisa Rasilimali Watu kutoka kampuni ya Sea Rock Resort Limited, Bariki Shayo, alisema kampuni hiyo imeshatekeleza baadhi ya makubaliano ikiwamo kukabidhi gari kwa kamati, ujenzi wa shule moja ya maandalizi na kuahidi kulipa stahiki zote kwa wafanyakazi waliosimamishwa kazi.

Aliwaomba wananchi hao kutekeleza makubaliano hayo kwa kuacha kutumia eneo la ufukwe na kuendelea kutumia eneo hilo kwa shughuli za uvuvi kuwa kunapunguza uingiaji wa wageni katika hoteli kutokana na mandhari chafu ya eneo hilo.

# Viongozi wa dini wataka maskini kupewa bima ya afya

**Na Mwandishi Wetu**

VIONGOZI wa dini na taasisi zisizo za kiserikali zimeiomba serikali kuangalia namna ya kusaidia wananchi maskini kupata matibabu kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF).

Maombi hayo yalitolewa na wadau wa Kamati ya Shirikisho la Imani nchini (ISCEJIC) kupitia mkutano uliofanyika Bagamoyo mkoani Pwani, uliolenga kujadili haki za kiuchumi na uadilifu.

Mkutano huo uliwakutanika wajumbe wa Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA), Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT) na Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), pamoja na mambo mengine walijadili masuala tofauti ya ufikiwaji wa huduma za kijamii ukilinganisha na maendeleo ya wananchi.

Askofu Joseph Mutorela wa CCT Dodoma, alisema suala la afya ni tatizo ambalo limekuwa likimpata kila mmoja, lakini wengi wao wamekuwa wakikosa uwezo wa kujitibia kutokana na kukosa kipato.

"Natambua kabisa serikali ina lengo jema katika kuhakikisha watu wake wanapoumwa wanatibiwa bila gharama kubwa, lakini upatikanaji wa bima ya afya kwao ni changamoto kutokana na wengi kukosa kipato cha kulipia tofauti na wafanyakazi au wenye kipato," alisema Askofu Mutorela.

Katibu wa Baraza la Ulamaa BAKWATA, Sheikh Hassan Chizenga, alisema pamoja na kwamba dini zimekuwa na mchango mkubwa wa kuombea watu wake na kuwaponya, lakini katika afya ya msingi serikali inapaswa kuangalia namna ya kusaidia watu wake wa hali ya chini wasiokuwa na uwezo, kwa kuwa gharama ya matibabu bado ni kubwa na wengi wanashindwa kumudu.

Mjumbe wa ISCEJIC, Prof. Tully Kassimoto, akizungumzia suala la jinsia na afya alisema wanawake na watoto ni waathirika, hivyo wanatakiwa kuangaliwa kwa ukaribu zaidi kwa kuwa ni tegemeo ndani ya familia.

Prof. Kassimoto alisema kama mama katika familia atakuwa na afya njema atazalisha na kuhudumia kwa ufasaha tofauti kama atakuwa mgonjwa shughuli zote za familia zitalala na hata watoto kukosa kupata chakula sahihi.




Moto ulioungu za maduka zaidi ya 10 na kuteketeza baadhi ya vitu katika majengo yanayomilikiwa na familia ya Nekemia Kazimoto (Kazikomu), yaliyopo Kata ya Kayanga Mjini, wilayani Karagwe, mkoani Kagera, juzi. **PICHA: ELIUD RWECHUNGURA**

# Waziri Gwajima aagiza madaktari bingwa kupelekwa mikoani

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, ameitaka mikoa yote nchini iweke utaratibu wa kuwaita madaktari bingwa ili kutoa huduma za kibingwa kwa wananchi katika mikoa hiyo.

Dk. Gwajima alisema kufanya hivyo kutawarahisishia wananchi kupata huduma karibu na maeneo yao pamoja na kupunguza idadi ya wagonjwa wanaopewa rufani ya kupelekwa katika hospitali nyingine.

Pia alisema kuwapo kwa utaratibu huo katika kila mkoa, kutasaidia kuokoa gharama kwa wananchi hao na kuwaondolea usumbufu.

"Nataka ratiba ya kila mkoa na kila halmashauri ya kuwaita madaktari bingwa kutokana na mzigo wa magonjwa uliopo kule na msiniambie kwamba hakuna hospitali au 'theatre' kwa sababu zote zimeshajengwa huko," alisema Dk. Gwajima.

"Mabingwa wenyewe ndio watajua namna ya kujipanga na kufanya utaratibu wao kwamba wanaanza kwenda wapi kutoa huduma hizo, isipokuwa kila halmashauri au mkoa unatakiwa kuwaambia wana kitu gani ambacho wanataka madaktari hao wakasaidie ili wao wajue namna ya kufanya."

Alisema badala ya pesa wanazopewa na wadau mbalimbali kwa ajili ya kuendeshea semina mbalimbali, ni vyema wakazitumia kupeleka huduma kwa wananchi.

"Tuna wadau wengi ambao wanatupeleka kwenye semina, tuwaombe badala ya semina hizo, watupatie pesa hizo tupeleke huduma kule kwa wananchi," alisema Dk. Gwajima.

Vile vile, siyo lazima kila mgonjwa anayefanyiwa vipimo apewe rufani ya kupelekwa katika hospitali nyingine.

"Siyo kila mtu anayefanyiwa vipimo lazima aende kule katika hospitali nyingine, vitu vingine vinaweza kumalizika hukohuko waliko," alisema.

# Taasisi za fedha zaombwa kufungua matawi Mtama

**Na Said Hamdani,** LINDI

BENKI zinazotoa huduma Mkoa wa Lindi zimeombwa kufungua matawi katika Halmashauri mpya ya Mtama, ili kuwaondolea wananchi tatizo la kutembea mwendo mrefu kufuata huduma za kifedha.

Kwa sasa wananchi wa Mtama hupata huduma za kibenki Manispaa ya Lindi, umbali wa zaidi kilomita (60), huku Benki ya NMB ikiwa imefungua tawi Kata ya Nyangao, umbali wa kilomita tano kutoka Mtama.

Ombi hilo limetolewa na wananchi wa halmashauri hiyo, kupitia Mbunge wa jimbo hilo, Nape Mnauye, wakati wa kikao cha kwanza cha kuapisha madiwani, kilichofanyika Kata ya Majengo, Mtama.

Nape aliwasilisha ombi hilo, kufuatia baadhi ya watendaji wa benki za CRDB, NMB, NBC na Posta kuwasili kwenye kikao hicho kwa ajili ya kuongeza wateja kupitia madiwani wa Halmashauri ya Mtama.

Alisema ili Mtama iweze kusonga mbele kimaendeleo, upo umuhimu kwa taasisi za kifedha kufungua matawi yao kuwaondolea wananchi adha ya kutembea mwendo mrefu wakiwa na fedha kufuata huduma zao mjini Lindi.

Alisema Rais Dk. John Magufuli, aliipatia Mtama hadhi ya kuwa halmashauri na kwamba upo umuhimu kwa taasisi za fedha kufungua matawi ili wananchi waondokane na tatizo hilo.

Alisema, pia kutawaondolea hofu ya usalama wa maisha yao ikiwamo kuporwa fedha zao na majambazi, huku akisisitiza benki itakayokuwa tayari kufungua tawi wataiunga mkono.

"Mimi nilishakutana na wakubwa wenu na kunieleza wanachokisubiri ni taarifa zenu, mkisema inafaa wao hawana kipingamizi," alisema Nape.

Wakipokea ombi la wananchi wa Mtama, watendaji wa benki hizo waliahidi kulifanyia kazi kwa manufaa ya wananchi wa Halmashauri ya Mtama.

Oktoba 15, mwaka huu, Rais Magufuli akiwa katika ziara ya Mkoa wa Lindi, ameibariki kwa kuitangaza Mtama kuwa halmashauri kamili.

**Pia kutawaondolea hofu ya usalama wa maisha yao ikiwamo kuporwa fedha zao na majambazi, huku akisisitiza benki itakayokuwa tayari kufungua tawi wataiunga mkono.**

## Wapanda milima 10 wafa kwa theluji Tehran

**Tehran,** IRAN

TAKRIBANI wapanda milima 10 wamefariki dunia na wengine kadhaa hawajulikani walipo katika milima ya Kaskazini mwa mji mkuu wa Iran, Tehran.

Tukio hilo ni baada ya theluji nzito kuanguka kutokana na upepo katika maeneo kadhaa ya Iran na kusababisha barabara kufungwa na kuathiri usafiri katika siku chache zilizopita.

Wapanda milima kadhaa hawajulikani walipo tangu siku ya Ijumaa, kuliporipotiwa vifo viwili huku idadi ya waliopotea ikihofiwa kuongezeka.

Tehran iko chini ya milima ya Alborz, ambayo ina hoteli nyingi za michezo ya kuteleza kwenye theluji.

Pia, mamlaka ya bahari ya Iran inawatafuta wafanyakazi saba wa meli ya usafirishaji ambayo imepinduka katika eneo la bahari la Ghuba, kulingana na shirika la habari la Iran, ISNA. **DW**

## Mataifa EU yaanza kutoa chanjo COVID-19

**Brussels,** UBELGIJI

MATAIFA ya Umoja wa Ulaya (EU), jana, yalianza kwa kutoa chanjo ya virusi vya corona kwa makundi ya watu walio kwenye hatari.

Hatua hiyo imeleta faraja kwenye mapambano dhidi ya mzozo huo wa kiafya kuwahi kushuhudiwa kwenye kanda hiyo.

Dozi za chanjo zimeanza kutolewa mapema kwa wafanyakazi wa huduma za afya, wazee pamoja na wanasiasa kadhaa kwa lengo la kuhakikisha umma kuwa chanjo ni salama.

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Czech, Andrej Babis, alipatiwa chanjo kwenye mji mkuu, Prague na kuwaambia raia wa nchi hiyo hawana sababu ya kuwa na hofu.

Akizungumza kwenye hospitali moja mjini Roma, Waziri wa Afya wa Italia, Roberto Speranza, alisifu mpango wa pamoja wa EU katika kutoa chanjo, akiwataka wakazi wa kanda hiyo kuendelea kuchukua tahadhari. **DW**



# Guterres: Dunia iangazie magonjwa ya binadamu, wanyama

**New York,** MAREKANI

KATIBU Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Gutteres, alisema jamii inahitaji kuangazia mwingiliano wa binadamu, mifugo na makazi ya wanyama, akisema asilimia 75 ya magonjwa mapya yanayoibukia ikiwamo ya kuambukiza yana uhusiano na wanyama.

Alisema katika hali hiyo, inafanya sayansi iwe mwongozo, uwepo wa mshikamano na uratibu baina ya nchi kwa kuwa hakuna aliye salama.

Guterres alisema hayo katika ujumbe wake wa siku hiyo iliyoadhimishwa jana, ikiwa ni mara ya kwanza.

Maadhimisho hayo yanafanyika huku janga la ugonjwa wa covid-19, likiwa limeshasababisha vifo vya watu zaidi ya milioni 1.7.

**Tunapohaha kudhibiti na kujikwamua kutoka katika janga la sasa, tunapaswa kufikiria siku za usoni. Bahati mbaya ni rahisi kufikiria virusi ambavyo vinaambukiza zaidi, lakini hatari zaidi.**

Guterres alisema mfumo wa UN pamoja na Shirika la Afya Duniani (WHO), uko thabiti katika kusaidia serikali na wadau wote katika kuimarisha maandalizi dhidi ya magonjwa ya milipuko.

Alisema mpango huo ni sehemu ya kazi za UN kujenga dunia yenye afya na hivyo kufanikisha Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs).

Guterres, alisema maadhimisho ya kimataifa ya siku ya kujindaa dhidi ya majanga, yamekuja katika kipindi ambacho ni muafaka na kuakisi ambacho kinapaswa kufanywa ili kuepuka madhara makubwa.

"Maadhimisho haya ya kwanza ya siku ya kimataifa ya kujiandaa kukabiliana na majanga yameangukia mwisho wa mwaka katika hali ambayo wengi walihofia na imetokea ni kweli ya kutisha," alisema Guterres.

Katibu Mkuu huyo, alisema Covid-19 imesababisha vifo, uchumi kusambaratika, jamii kuwa hatarini kuwahi kutokea.

"Tunapohaha kudhibiti na kujikwamua kutoka katika janga la sasa, tunapaswa kufikiria siku za usoni. Bahati mbaya ni rahisi kufikiria virusi ambavyo vinaambukiza zaidi, lakini hatari zaidi," alisema Katibu Mkuu.

"Jamii zinahitaji mifumo thabiti ya afya, ikiwamo huduma ya afya kwa wote. Nchi zinahitaji hifadhi zaidi ya kijamii. Jamii zilizo mstari wa mbele zinahitaji usaidizi. Nchi zinahitaji msaada fanisi zaidi wa kiufundi," alisema.

Alisema ujumbe; uwezo wa kujikinga uongezwe ili dunia ikabiliane na mlipuko mwingine. **UN**



Mhamiaji akitembea kwenye theluji huku amejifunika blanketi katika kambi ya Lipa Kaskazini Magharibi mwa Bosnia, karibu na mpaka na Croatia, mwishoni mwa wiki. Mamia ya wahamiaji wanakumbwa na baridi huku theluji nzito ikianguka ikiwa ni majira ya baridi na hali mbaya ya hewa. **PICHA: AP**

# Kikosi cha usalama India chashutumiwa mauaji raia

**Mymensingh,** BANGLADESH

KIKOSI cha Usalama Mpaka wa India (BSF) kinashutumiwa kwa mauaji ya raia katika maeneo ya mpaka wa Bangladesh.

Mfugaji wa Bangladesh mwenye umri wa miaka 45, Khairul Islam, aliuawa na kikosi cha BSF, Desemba 22 katika mji wa Mymensingh, ulioko mpakani mwa Bangladesh.

Wakati mazungumzo yakiendelea kati ya nchi hizo mbili juu ya kusitisha mauaji ya raia katika eneo la mpakani, mwathirika wa mwisho alikuwa ni Islam ambaye ni baba wa watoto watatu.

Dulal ambaye ni mdogo wake Islam, alisema kuwa kaka yake aliuawa na kikosi cha BSF, ingawa alikuwa raia wa kawaida ambaye hakuwa na silaha yoyote.

Dulal aliongezea kusema kuwa walimpeleka kaka yake hospitalini lakini hawakuweza kumwokoa, na kwamba vikosi vya usalama vya India vilifunga tukio hilo bila kutoa hukumu ya aina yoyote.

Kikosi cha BSF kiliwaua raia 15 wa Bangladesh mwaka 2018, raia 43 mwaka 2019 na raia wasiopungua 35 mwaka huu na kuwajeruhi raia wengine 22.

Baada ya mazungumzo kati ya mamlaka ya kikosi cha BSF na Bangladesh juu ya utumiaji mbaya wa silaha katika maeneo ya mpakani, maofisa wa kikosi hicho cha BSF walitoa ahadi yao tena ya kutotekeleza mauaji katika maeneo ya mipaka.

Kwa upande mwingine, vikosi vilijitolea kupanua ushirikiano wa kudhibiti uhalifu wa mipaka, na kuamua kushika doria za pamoja katika maeneo ya mpakani, ili kukomesha visa vya mauaji. **TRT**

# GUARDIOLA ASIFIA KIWANGO MAN CITY



**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amekipongeza kikosi chake cha Manchester City kwa ushindi dhidi ya Newcastle United, akielezea kwamba, matokeo hayo ya 2-0 yalibebwa na "kiwango bora cha msimu".

City ilipata ushindi rahisi dhidi ya Newcastle shukrani kwa mabao kutoka kwa Ilkay Gundogan na Ferran Torres na sasa wamepitwa pointi tano tu na vinara wa ligi hiyo, Liverpool, baada ya mchezo huo wa Jumamosi.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Guardiola aliwaambia waandishi wa habari: "Kilikuwa kiwango bora cha msimu.

"Soka letu lilikuwa bora kabisa, timu ilicheza kwa kiwango cha kuvutia na tulionyesha tuna njaa ya ushindi.

"Kiwango cha leo (juzi) kwa uhakika kabisa kilikuwa bora sana, kwani timu ilicheza kwa kuonyesha ubunifu na wa hali ya juu."

City imeshinda mechi zote saba katika mashindano yote ambapo Torres ndiye amekuwa mfungaji wao, tano kati ya saba wamecheza kwenye dimba la Etihad.

# Rashford ajiwekea rekodi ya mabao EPL

**MANCHESTER,** England

MARCUS Rashford ameingia kwenye rekodi ya kuwa mchezaji wa tatu kufikisha idadi ya mabao 50 kwenye Ligi Kuu England katika umri mdogo zaidi.

Rekodi hii inamweka nyuma ya watangulizi wake Wayne Rooney na Cristiano Ronaldo.

Rashford alifikia rekodi hiyo ya mabao baada ya kufunga goli la kwanza kwenye mechi dhidi ya Leicester City, Jumamosi.

Goli hilo lilikuwa la sita kwa Rashford msimu huu, lililowatanguliza Man United kifua mbele.

Alifunga bao hilo akiwa na umri wa miaka 23 na siku 56 na sasa anashika nafasi ya tatu kwenye orodha ya wachezaji waliofunga idadi hiyo ya mabao kwenye EPL.

Rooney ambaye ndiye anashikilia rekodi hii katika nafasi ya kwanza, alifikisha idadi hiyo ya mabao akiwa na umri wa miaka 22 na siku 157 pale United, wakati Ronaldo ambaye anashikilia nafasi ya pili alifikisha idadi kama hii akiwa na umri wa miaka 22 na siku 341.

Rashford amekuwa sehemu muhimu ya mafanikio ya United tangu alipowasili klabuni hapo.

Amefunga jumla ya mabao 17 na kutoa usaidizi wa magoli 13, huu ni uwiano wa mabao 30/59 yaliyopatikana akiwapo klabuni hapo.





# Alonso awindwa Atletico Madrid

**MADRID,** Hispania

KLABU ya Atletico Madrid imeripotiwa kuwa wanamtupia jicho mlinzi wa Chelsea, Marcos Alonso katika uwezekano wa kumwongeza kikosini wakati wa dirisha dogo la usajili la Januari.

Licha ya kukaa kileleni mwa msimamo wa LaLiga, kocha wa Atletico, Diego Simeone, ataingia sokoni katika dirisha la Januari ili kuimarisha safu yake ya ulinzi.

Kocha huyo raia wa Argentina pia anataka kuwa na machaguo ya kutosha linapokuja suala la mabeki wa pembeni, jambo ambalo linaonekana kuwapa Atletico pia nafasi ya kutaka kumsajili, Ainsley Maitland-Niles wa Arsenal.

Kwa mujibu wa El Chiringuito, Simeone pia anamtamani Alonso, ambaye anatarajiwa kuondoka Stamford Bridge mwezi ujao.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, hajapata nafasi ya kuichezea Chelsea tangu mechi waliyotoka sare ya mabao 3-3 ugenini dhidi ya West Bromwich Albion, Septemba 26, akiendelea kuwa nyuma Ben Chilwell na Emerson Palmieri.

Atletico inasemekana wanaandaa mazingira ya kujadili mkataba wa mkopo na klabu yake hiyo ya Ligi Kuu England.

HABARI MICHEZO

# Mbappe aitemea nyongo Cameroon

**PARIS,** Ufaransa

NYOTA wa Ufaransa na Klabu ya Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe, amezijia juu taarifa ya watu wengi kwenye mitandao ya kijamii inayosema yeye ni raia wa Cameroon na si Ufaransa.

Mbappe amejibu shutuma hizo na kusisitiza yeye ni raia halali wa Ufaransa na si Cameroon.

"Mimi siyo ria wa Cameroon. Mimi ni Mfaransa," alisema Mbappe akinukuliwa na jarida na France Football.

"Mwanzoni kabisa wakati nimeanza kujihusisha na soka, wakati bado kiza kimetanda mbele yangu, baba yangu aliwasiliana na 'Fecafoot' ili waweze kunipa nafasi ya kuchezea timu ya Taifa ya Cameroon.

"Wakamtaka atoe kiasi kikubwa cha fedha ili mimi niweze kuchezea timu hiyo. Baba yangu ambaye hakupendezwa na kitendo hicho akaamua kuhamishia majeshi Ufaransa, Ufaransa hii ambayo imenipa nafasi ya kuuonyesha ulimwengu uwezo nilionao katika soka.

"Sasa leo nimekuwa mchezaji mwenye gharama zaidi duniani, ndipo Cameroon wananipigia simu na kunipa utaifa ambao si wangu.

"Mimi ni Mfaransa na nitabaki kuwa raia wa Ufaransa," alisema Mbappe.

Ikumbukwe Kylian amezaliwa katika kitongoji cha Bondy, Kaskazini Mashariki mwa Jiji la Paris nchini Ufaransa.

Wazazi wake ni Wilfried Mbappe (ambaye alikuwa kocha wa mpira) na mama yake raia wa Algeria, Fayza Mbappe.







# FABINHO ATAKA TAJI LA PILI

**LIVERPOOL,** England

FABINHO amekiri kwamba, Liverpool wakipata taji la pili la Ligi Kuu England, litakuwa muhimu na la kipekee zaidi ya lile lililopita kwenye kumbukumbu nzuri ya soka.

Liverpool walitwaa taji lao la kwanza la Ligi Kuu baada ya miaka 30 msimu uliopita, baada ya kuwatupa mbali kwa pointi 18 Manchester City waliokuwa wakitetea taji hilo.

Msimu huu umekuwa mgumu, na ni mwendelezo wa changamoto zilizoanza tangu msimu uliopita, huku janga la corona likiwa ni tatizo kubwa zaidi lililokwamisha sana shughuli za soka.

Msimu huu Liverpool wamekuwa na changamoto ya majeruhi, wakimkosa mlinzi wao wa kati, Virgil Van Dijk na pia Joe Gomez kwa kipindi fulani.

Lakini Fabinho anaamini kuwa ikiwa watashinda kwa mara nyingine taji la Ligi Kuu England, basi hili litawapa heshima kubwa zaidi na litakuwa taji la kipekee kwenye historia ya klabu.

"Ukizingatia kila kitu kilichotokea mwaka huu, ugumu wote wa kutokuwa na mashabiki uwanjani na ratiba ngumu za mechi na majeruhi, yote haya yanafanya taji la pili kuwa la kipekee zaidi kuliko lile la awali," alisema Fabinho akinukuliwa na Sky Sport.

# Alaba kupotezewa Manchester United

**MANCHSTER,** England

MANCHESTER United wameripotiwa kuwa na uwezekano wa kutemana na mpango wa kuwania kumsajili mlinzi wa Bayern Munich, David Alaba wakati wa dirisha dogo la usajili la Januari.

Nyota huyu amesalia na miezi sita tu kwenye mkataba wa sasa na raia huyo wa Austria anaweza kufanya mazungumzo rasmi na klabu yoyote inayomhitaji kuanzia mwezi ujao.

Man United, pamoja na klabu nyingine kubwa za Ulaya zimehusishwa sana na uhamisho wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28. Kwa mujibu wa wa gazeti la Telegraph, kocha Ole Gunnar Solskjaer anapinga mpango wa kufanya nyongeza yoyote kikosini katikati ya msimu.

Msimamo huu wa United unaweza kuwapa faida wapinzani wake katika kuinasa saini ya staa huyu. Bila shaka anaweza kujikuta anakuwapo Allianz msimu wote au akashawishika kuhamia klabu nyingine.

Hata hivyo, Alaba bado ni sehemu muhimu ya mabingwa hawa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, akiwa amecheza jumla ya mechi 18 kwenye mashindano yote tangu Septemba mwaka huu.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ARTETA AFUNGUKA USHINDI CHELSEA

Kwa uhakika kabisa ulikuwa ushindi mzuri kwetu, tulipagawa na kukatishwa tamaa...

**LONDON,** England

MIKEL Arteta ameutaja ushindi wa Arsenal dhidi ya Chelsea kama ni "maalumu" baada ya timu hiyo kumaliza ukame wa mechi saba bila kushinda kwenye Ligi Kuu England.

**Arsenal ilimaliza Sikukuu ya Krismasi vizuri, huku mabao ya Alexandre Lacazette, Granit Xhaka na Bukayo Saka yakiwawezesha kupata ushindi wa 3-1, juzi Jumamosi.**

Chelsea ilipata bao la kufutia machozi kupitia kwa Tammy Abraham, huku Jorginho akikosa penalti iliyookolewa na golikipa, Bernd Leno.

Ushindi huo umeinyanyua Arsenal hadi nafasi ya 14 kwenye msimamo wa ligi, mbele ya Brighton and Hove Albion na West Brom.

"Kwa uhakika kabisa ulikuwa ushindi mzuri kwetu sisi," alisema Arteta anikunukuliwa na Sky Sports.

"Tulipagawa na kukatishwa tamaa kutokana na matokeo tuliyokuwa tukiyapata, na si kiwango. Wachezaji walikuwa kwenye wakati mgumu, mashabiki wetu walikuwa wanaumia.

"Leo ni siku maalumu. Imekuwa siku nzuri ya Boxing Day, kucheza kwenye 'dabi' ya London katika dimba la Emirates, na kushinda kwa namna tulivyoshinda.

"Matumaini yangu hii ni njia sahihi ya kurekebisha pale tulipokosea, sasa itakwenda kufanya mabadiliko ya kiwango kwa timu nzima.

"Najua kwamba wanaweza kucheza kwa kiwango kama cha leo (juzi), inaonyesha ni namna gani mambo yanaweza kubadilika kwa haraka sana kama tu tukiamua kucheza kwa kujituma.

"Kwa wakati huu mchezo ulikuwa mzuri na mgumu, lakini tulikuwa bora zaidi na tukapata matokeo mazuri."

## ZISIKUPITE

### FODEN AWANIWA MADRID

KIUNGO wa Manchester City, Phil Foden, anawaniwa na Real Madrid, ambao wanaamini wanaweza kupata saini yake kwa sasa, kwa sababu nyota huyo mwenye umri wa miaka 20 hana nafasi ya kucheza mara kwa mara. ***(Sunday Mirror)***

### JUVENTUS WAMKAZIA POGBA

JUVENTUS inafikiri kumrudisha kiungo, Paul Pogba Januari kule Turin, lakini watatakiwa kusubiri hadi Manchester United ikubali ofa yao ya pauni milioni 50 kwa ajii ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27. ***(Eurosport)***

### LEEDS WAMTAKA JOHNSTONE

GOLIKIPA wa West Brom, Sam Johnstone, mwenye umri wa miaka 27, anaweza kuwaniwa na Leeds na Brighton kama timu yake ikishuka daraja kutoka Ligi Kuu England. ***(Sun on Sunday)***

### OZIL AIGAWA ARSENAL

KIKOSI cha kwanza cha Arsenal kimegawanyika kutokana na kutemwa kwa kiungo Mesut Ozil mwenye umri wa miaka 32, huku kundi kubwa la wachezaji wakubwa wakimsapoti raia huyo wa Ujerumani. ***(Sunday Telegraph)***

### PSG KUMTOA PEREDES

KLABU ya Paris St-Germain itakuwa tayari kuwapa ofa Inter Milan ya kiungo wao, Leandro Paredes, 26 raia wa Argentina, ili kubadiishana na kiungo, Christian Eriksen, 28. ***(Le10Football)***

### NUNO AMTETEA TRAORE

KOCHA wa Wolves, Nuno Espirito Santo, amemtetea mchezaji wake, Adama Traore, 22, baada ya winga huyo kutokuwa kwenye kiwango kizuri msimu huu. ***(Sunday Mirror)***

### WOLVES YAMUWANIA JOVIC

KLABU ya Wolves inaweza kutaka kumsajili straika wa Real Madrid, Luka Jovic mwenye umri wa miaka 22, au mshambuliaji wa Liverpool, Divock Origi, 25, ili kuimarisha safu yao ya ushambuliaji. ***(Express & Star)***

### BENITEZ KUMRITHI ARTETA

KOCHA wa zamani wa Liverpool na Newcastle, Rafael Benitez, anaweza kuwaniwa na Arsenal kama klabu hiyo itaamua kumfukuza Mikel Arteta. ***(Sunday Express)***

### SPURS YAMTAKA SABITZER

KLABU ya Tottenham Hotspur inawania kumsajili kiungo wa RB Leipzig, Marcel Sabitzer, 26, huku timu hiyo ya Ujerumani ikiwa bado haijathibitisha kumwongezea mkataba wake unaomalizika kipindi cha majira ya joto mwaka 2022. ***(Bild's Christian Falk on Twitter)***

### JAMES AGOMBEWA ENGLAND

WEST Brom imeungana na Leeds, Burnley na Brighton kuwania kumsajili kwa mkopo winga wa Manchester United, Daniel James mweye umri wa miaka 23, wakati wa dirisha dogo la Januari. ***(Daily Star Sunday)***

HABARI MICHEZO

## Mfaume atoa siri kumpiga Mmalawi

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI Bondia wa ngumi za kulipwa nchini, Mfaume Mfaume, akitetea mkanda wake wa ubingwa wa Afrika (ABU) baada ya kumpiga mpinzani wake, Chikonda Makawa kutoka Malawi katika pambano la usiku wa mabingwa lililofanyika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, ametoa siri ya ushindi huo.

Akizungumza na gazeti hili baada ya mpambano huo ambao uliwakutanisha mabondia kutoka nchi mbalimbali, alisema licha ya kushinda mpinzani wake alikuwa na uwezo mkubwa.

Mfaume alisema siri ya ushindi huo ni mazoezi ya muda mrefu aliyokuwa akiyafanya kwenye kambi aliyokuwa ameiweka Ifakara mkoani Morogoro.



Alisema amefurahi kupata ushindi huo huku akiwashukuru Watanzania wote pamoja na wadau mbalimbali waliojitokeza kumuunga mkono.

"Mpambano ulikuwa na ushindani mkali kwani nimepigana na bondia mwenye uwezo mkubwa kwa sababu alikuwa anajua kujilinda vema ulingoni," alisema Mfaume.

## Usafiri waahirisha michuano Taifa Cup

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya Taifa Cup ya mchezo wa Netiboli yaliyokuwa yaanze leo Manyara, yamesogezwa mbele mpaka Januari 3, mwakani kutokana changamoto ya usafiri wa kuelekea mkoani humo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Chama cha Netiboli Tanzania (Chaneta), Devota Marwa, alisema, licha ya changamoto hiyo mpaka sasa timu 12 ndizo ambazo zimethibitisha kushiriki mashindano hayo.

Mwenyekiti huyo aliitaja mikoa ambayo imethibitisha kushiriki ni Simiyu, Geita, Mwanza, Mara, Mbeya, Dodoma, Singida, Arusha, Dar es Salaam Pamoja na wenyeji Manyara.

"Tulitarajia kuwa na timu ishirini, lakini mpaka sasa hazijakamilika wengi wanalalamika hawana nauli, lakini nafasi mpaka sasa bado zipo," alisema Devota.

Alitoa wito kwa timu na mikoa ambayo itakuwa tayari kushiriki itoe taarifa mapema ili ziweze kupangwa kwenye ratiba kabla kalenda ya mashindano hayo kutoka.

Alisema mwisho wa kuthibitisha kushiriki ni Januari Mosi, mwakani na baada ya hapo hawatapokea maombi yoyote kwani muda utakuwa umekwisha.

# NTIBAZONKIZA AONGEZA MZUKA MABAO YANGA




**Na Mwandishi Wetu**

UWEZO binafsi wa ingizo jipya ndani ya kikosi cha Yanga, Mrundi Said Ntibazonkiza, umezidi kuongeza ari ya kufanya vizuri kwa wachezaji wenzake hususan katika safu ya ushambuliaji.

**Safu ya ushambuliaji ya Yanga ilikuwa ikiandamwa na ukame wa mabao na katika mechi nyingi za Ligi Kuu ilikuwa ikiibuka na ushindi wa bao moja, lakini sasa imeanza kupata ushindi mnono.**

Ntibazonkiza ameonyesha uwezo mkubwa wa kutoa pasi za mwisho na kufunga pia kwa mipira 'iliyokufa', hatua ambayo imepokelewa vizuri na washambuliaji wenzake

Michael Sarpong ambaye hadi sasa amefunga mabao manne licha ya kupewa nafasi zaidi katika kikosi hicho msimu huu, amesema sasa atazitumia vema nafasi zinazotengenezwa na Ntibazonkiza kufunga mabao.

Sarpong amemwambia mwandishi wetu kuwa, kitendo cha kuwa na mchezaji wa aina kama Ntibazonkiza kikosini, ni faida kwao na kwamba atahakikisha anatumia umbo lake vizuri kwa kufunga mabao ya kutosha hususan kutumia mipira ya faulo inayopigwa na Mrundi huyo.

"Kikubwa ni kuisaidia timu kupata matokeo na ndiyo jukumu la kila mchezaji ndani ya kikosi chetu kwa sababu tunahitaji mafanikio ya pamoja, kupambana kunatokana na mchango wa kila mmoja kama unavyoona kwa Ntibazonkiza.

"Ni mchezaji mzuri ambaye kwetu atatusaidia kutokana na uzoefu na ubora alionao, lakini kwangu nataka kuona natumia vizuri ubora wake hasa katika mipira ya faulo kuhakikisha nafunga mabao ambayo yatatusaidia kufikia malengo," alisema.

SASA RASMI...




Beki wa kati wa zamani wa Yanga, Kelvin Yondani, akionyesha uzi atakaotumia baada ya kutambulishwa rasmi kujiunga na timu ya Polisi Tanzania katika dirisha hili dogo linalotarajiwa kufungwa Januari 15, mwakani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## *Azam yazindukia FA Cup kwa Magereza*

**Na Mwandishi Wetu**

KIKOSI cha Azam FC kimetinga hatua nne kwenye mchezo wa Kombe la Shirikisho baada ya juzi kuibuka ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Magereza FC.

Ushindi huo pia umeongeza ari ya kufanya vizuri kwa timu hiyo ambayo imekuwa katika wakati mgumu wa kushinda kwenye Ligi Kuu Bara.

Alhamisi wiki hii, Azam ambayo ipo nafasi ya tatu kwenye msiamo wa Ligi Kuu Bara, itakuwa ugenini katika Uwanja wa Ushirika mjini Moshi, kuvaana na wenyeji wao, Polisi Tanzania kwenye mechi ya mzunguko wa pili wa ligi hiyo.

Ushindi huo wa juzi dhidi ya Magereza FC ambao ni wa kwanza kwa kocha George Lwandamina tangu aanze kuinoa timu hiyo takriban wiki tatu sasa, unampa mwanga wa mafanikio na kuongeza ari ya kupambana kwa wachezaji wake.

Mashabiki wa Azam FC walishuhudia mabao hayo yakipachikwa na Obrey Chirwa dakika ya 24 na Never Tigere dakika ya 65.

Azam iliugawa mchezo kwa vipindi viwili ambapo kipindi cha kwanza Chirwa alipachika bao hilo kwa kichwa akitumia kona ya Never Tigere.

Kipindi cha pili Azam ilipata bao kupitia kwa Tigere ambaye amekuwa nyota wa mchezo huo akihusika kwenye mabao yote mawili, akifunga moja kutoa pasi moja iliyozaa bao.

Michuano hiyo iliendelea jana kwa mabingwa watetezi, Simba kuikaribisha Majimaji FC katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

# Michezo

Jumatatu Desemba 28, 2020

Nipashe




Arteta afunguka ushindi Chelsea UKURASA 22

SIKU YETU...



Bukayo Saka (wa pili kushoto) akipongezwa na wachezaji wenzake wa Arsenal baada ya kuifungia timu yake bao la tatu wakati ikishinda 3-1 dhidi ya Chelsea kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Emirates juzi. **PICHA: MTANDAO**

# SVEN NA HESABU KALI SIMBA KWA PLATINUM

●●● Kuanza kutesti mitambo akiikaribisha Ihefu FC kwenye Ligi Kuu Jumatano, huku akieleza...

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya jana kushuka dimbani kuanza mkakati wa kutetea taji lao la Kombe la Shirikisho (FA Cup), hesabu zote za Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Sven Vandenbroeck, amezielekeza katika mechi ya marudiano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya FC Platinum.

**Simba ilikubali kipigo cha bao 1-0 ugenini nchini Zimbabwe kwenye mechi hiyo ya kwanza ya raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa, hivyo inahitaji ushindi kuanzia mabao 2-0 ili kutinga hatua ya makundi ya michuano hiyo yenye utajiri mkubwa kwa ngazi ya klabu barani Afrika.**

Timu hizo zitarudiana Januria 6, mwakani, lakini kabla ya hapo Simba itakuwa na kibarua kingine keshokutwa, Jumatano itakapoikaribisha Ihefu FC kwenye mechi ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Bara.

Simba ambayo hadi sasa imeshuka dimbani mara 14, ipo nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 32, huku Yanga ikiwa kileleni na alama zake 43 zilizotokana na mechi 17. Sven ameweka wazi kuwa, anaamini watafuzu hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika katika mchezo wa pili wa michuano hiyo dhidi ya FC Platinum utakaopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

"Bado tuna nafasi kubwa ya kufuzu hatua ya makundi licha ya kupoteza mchezo wa kwanza, tunaamini tutapata matokeo mazuri katika mechi ya marudiano tukiwa kwenye uwanja wa nyumbani.

"Tunaendelea kufanya maandalizi ya nguvu kwa sababu hatukupoteza mchezo wa kwanza kutokana na ubora wa wapinzani bali imetokea kutokana na makosa ambayo tulifanya," alisema.

Sven alisema wanachokiangalia kwa sasa ni mchezo wa pili, wakiwa nyumbani, jambo ambalo anaamini watakuwa na nguvu kubwa ya kupambana na kuweza kupindua matokeo.

"Kikubwa kwa sasa ni kuangalia timu inataka nini kiufundi baada ya kuwaona wapinzani wetu, tunataka matokeo makubwa nyumbani," alisema Sven.

Simba kwa sasa ipo katika presha kubwa ya kushinda mechi hiyo ili kufuzu hatua ya makundi, lakini kuhakikisha haipotezi pointi kwenye michezo yake ya Ligi Kuu ili kuweza kupunguza wigo wa pointi dhidi ya Yanga iliyopo kileleni.

Endapo Simba itashinda mechi zake zote za ligi, itafikisha pointi 41, mbili nyuma ya Yanga, hivyo kuendelea kutoa upinzani katika mbio za kutetea ubingwa wake, wakati huu ikitaka kutwaa taji hilo kwa mara ya nne mfululizo.

# Prisons yatamba kuitibulia Yanga

**Na Adam Fungamwangp**

KLABU ya Prisons imesema kuwa imejipanga kulipa kisasi kwa Yanga, cha kuwaharibia rekodi yao ya kutopoteza mechi hata moja kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliopita, na sasa ikidai kuwa ni zamu yao.

Katibu Mkuu wa Prisons, Ajibu Kifukwe, amesema anakumbuka msimu uliopita Prisons ilikuwa ndiyo timu pekee ambayo haijapoteza mechi hata moja kwenye Ligi Kuu, lakini Yanga ndiyo ilitibua rekodi hiyo, kwa hiyo na wao wamejipanga kulipiza kisasi kwa kuwaharibia rekodi yao ya kutopoteza pia.

"Yanga haijapoteza mechi, sisi tumejipanga kuwa timu ya kwanza kuifunga na kuharibu rekodi hiyo kama walivyotufanyia wao msimu uliopita," alisema Katibu huyo.

Msimu uliopita, Prisons ilikuwa ndiyo timu pekee kwenye Ligi Kuu ambayo ilicheza mechi 12 bila kupoteza, kabla ya kufungwa bao 1-0 dhidi ya Yanga.

Baada ya kushinda mechi nne na kutoka sare nane, Prisons ilichapwa bao 1-0 kwenye Uwanja wa Samora mjini Iringa Desemba 27, mwaka jana kwa bao la Mnyarwanda, Patrick Sibomana.

Alisema anaamini kuwa mechi haitokuwa rahisi, lakini na wao pia ni timu nzuri na wamejipanga kukabiliana na Yanga ambayo imemaliza mzunguko wa kwanza bila kupoteza mechi hata moja, ikicheza mechi 17, ikishinda 13 na kutoka sare nne na ndiyo inayoongoza kwenye msimamo wa ligi mpaka sasa.

Desemba 31 kwenye Uwanja wa Nelson Mandela mjini Sumbawanga, Prisons yenye pointi 21 ikiwa nafasi ya 11, inatarajia kuikaribisha Yanga kwenye mechi ya kwanza ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042